# Kama Nilivyokuwa Pamoja Na Musa, Ndivyo Nitakavyokuwa Pamoja Na Wewe

Jeffersonville, Indiana, Amerika
Septemba 11, 1960A

1 1…nje tena asubuhi hii, baada ya kulala vizuri usiku. Natumaini wote tulikuwa nao na tunajisikia kupumzika leo. Nilikuwa tu nikiwaza, nilipokuwa nimesimama chumbani na…. Billy Paul aliweka senti ishirini na tano asubuhi ya leo. Ninakumbuka nikiwa nimesimama juu ya hii miimbara wakati Frankie Weber….. Jirani hapa, yeye na mimi tulienda shule pamoja. Na nilikuwa na kama miaka ishirini na moja hivi, au ishirini na mbili hivi, ninaamini, naye alikuwa tayari na miaka ishirini na tano. Na alipoweka senti ishirini na tano nilifikiria, "Ee, jamani, Frankie ni kama yuko tayari kufa, yeye ni mzee." Na sasa….Nikawaza, "Nitafanya nini nitakapofikia umri huo, miaka ishirini na tano?" Na sasa mwanangu anaweka senti ishirini na tano.

Linakwenda tu kuonyesha kwamba muda unakimbia na haumsubiri yeyote. Ni lazima tufanye kazi kungali mchana, kwani wakati utakuja ambapo hatutaweza kufanya kazi tena. Na wakati wote nilipenda *Zaburi ya Maisha* ya Longfellow, "Pamoja na kuachana, tunaacha nyuma yetu alama za nyayo kwenye mchanga wa wakati." Ni lazima tuache alama za nyayo wakati ambapo tunaweza kuacha, kila mmoja wetu. Hebu na tusiipoteze siku moja, lakini tufanye kila siku iwe bora tuwezavyo kwa ajili ya utukufu Wake.

2 Siku kadha zilizopita, au wiki mbili zilizopita, imekuwa…. Bwana hutoa maono, kama wote tulivyo na uhakika wa hayo hapa. Na nilikuwa na ona la ajabu kunitokea wakati nilipokuwa huko Kentucky. Nilisema kwa wale niliokuwa nao, "Kitu fulani hakika kinajiandaa kutokea."

Niliona akisimama mbele yangu, kiasi cha saa tisa kamili alfajiri chumbani, mtu fulani, mweusi wa kutisha. Siyo kama ndugu zetu na dada wapenzi weusi; huyu mtu alikuwa tofauti. Mwili wake ulikuwa kama chuma chenye makunyanzi, na alikuwa akija kunikamata na mikono mikubwa, na ulinzi wangu ulikuwa wembe mdogo. Lakini haukufaa, usingeweza … kujilinda mwenyewe na huo. Hivyo, kwa namna fulani Bwana aliingia na kunisaidia kumkimbia huyo mtu wa kutisha. Alikuwa chuma chenye makunyanzi. Ningeweza kumwona alivyokuwa akiinua mikono yake, makunyanzi makubwa katika ngozi yake, kama tu chuma kikitembea mbele na nyuma. Nadhani, labda, risasi ya yenye nguvu isingeweza kutoboa hilo gamba la kutisha (kama ya mnyama fulani, kobe au kitu fuani) juu yake. Na alikuwa akinifuata. Nilikuwa na wazo zuri hicho kilikuwa nini na kilimaanisha nini.

3 Lakini basi Jumanne iliyopita asubuhi, takriban saa tatu kamili, kitu fulani kingine kilitokea. Nilikuwa nyumbani, na aliyekuwa amesimama mbele yangu alikuwa yule wa Kiungu ambaye alinena maneno ambayo sikuyaelewa. Na ule wakati aliouweka ulikuwa umekaribia sana. Na sikumsikia vizuri sana, lakini alikuwa wa Kiungu. Na alisema, "Siku saba zaidi, na utasimama kama Musa alivyosimama," au "utakuwa kama Musa alivyokuwa," au kitu fulani kuhusu Musa. Hilo linaniacha siku moja zaidi baada ya leo. Hiyo ilikuwa ya sita. Sijui hilo linamaanisha nini. Ninajua kwamba Yeye atalifanyia kazi, chochote linachomaanisha. "Utasimama," au "utapaswa kusimama," au "kuwa kama," au …. Ilikuwa kitu fulani kinachohusiana na Musa. Na kamwe sikukiwazia. Niliiambia familia yangu na kuwaambia baadhi ya wapenzi wangu kwamba nilimwona huyu wa Kiungu. Bado, yeye alinena kama mwanadamu.

Na kisha niliona kwamba ujumbe wangu wa jioni iliyopita, Bwana aliniruhusu nimchague Musa. Na asubuhi ya leo ni Musa na mrithi wake. Na Maandiko ambayo ninakaribia kuyaendea asubuhi hii ni kuhusu Musa na Yoshua. Na haya Maandiko, Yoshua sura ya kwanza, siku zote yamekuwa ni Maandiko muhimu sana. Sijawahi kamwe kuhubiri hayo maishani mwangu; ninakwenda kuyajaribu asubuhi hii.

4 Lakini kiasi cha miaka miwili iliyopita, niliona Biblia, chumbani, ikishuka chini na kusimama nilipokuwa. Na mkono kutokea juu ulishuka chini na kufungua kurusa, ulizifungua; na kushuka chini, Yoshua 1 hadi kwenye aya ya tisa, na kusimama, ukienda taratibu. Nimekuwa nikisubiri huu wakati ukaribie, wakati ambapo ningejisikia kwamba yalikuwa ni mapenzi ya Mungu kwangu kunena juu ya hilo.

Sasa msisahau ibada za jioni, kama mnaweza kuja na kama hamko kazini, Kama mna makanisa yanayowahitaji, mbona, sisi tunawashauri mwende kwenye makanisa yenu.

Asubuhi hii tutaenda kuwaombea wagonjwa, mara tu baada ua ujumbe. Na ninafikiri kuna, kufuatia hilo, ni ibada ya ubatizo.

Na usiku huu, Bwana akipenda, nataka kuhubiri juu ya *Vitambulisho Vitano vya Kimaandiko Vya Kanisa Visivyoshindwa*, na uhusiano wetu na hivyo-na Kanisa la Agano Jipya, na uhusiano wetu na kanisa hili. Na ibada zitaanza, ibada ya nyimbo, saa moja na nusu; nitajaribu kuwa kwenye mimbara saa mbili kamili. Na tutakuwa tumemaliza penye saa tatu na nusu, Bwana akipenda.

5 Na kisha natumaini kwamba leo kwamba haitakuwa mojawapo ya haya maneno kwamba … wakati ninakuja kwenye hilo agizo, kwamba hakuna mmoja ambaye atashindwa kuliona, kwa sababu ni muhimu sana kwamba utaweka kando kila kitu sasa na kuwaza, tunapomngojea Roho Mtakatifu.

Kabla ya kuliendea hili Neno la ajabu na la thamani, ninaenda kumwomba yule rafiki yangu mwema na mtenda kazi pamoja nami, Dr. Lee Vayle, kama atasimama na kutuongoza katika neno la maombi, tunapolifungua Neno. Ndugu Vayle. [Ndugu Vayle anaomba.] Asante, Ndugu Vayle, kwa hayo maombi yenye kuvuvia kwa Mungu.

6 Na sasa hebu tufungue katika Maandiko. Yapo mengi sana ya kuongelea, lakini bado ninappona wengi wakiwa wamesimama kuzunguka kuta na ndani ya kuta, na kadhalika. Ninaamini tunaelekea kupambazuka kwa siku mpya. Sasa, katika kusomwa kwa Maandiko asubuhi hii, hebu tufungue ile sura ya kwanza wa Yoshua. Na tutasoma kutoka katika kitabu cha kwanza cha Yoshua, sura ya kwanza, aya tisa za kwanza.

Wakati tukijiandaa…. Huu ujumbe unarekodiwa, na utatumwa sehemu nyingi za ulimwengu. Ningependa watu wa ulimwengu ambao Mungu amenipa kibali na nimepata neema mbele zenu, ninasema hili asubuhi hii kwa sababu kwamba siku za mbeleni natumaini kuja kwenye makusanyiko yenu katika mikutano, kwamba mweze kujua mapema kile ambacho Bwana Mungu amefanya, ili mweze kujua ukweli. Na kama Yesu alivyosema, "Kweli itawaweka huru."

7 Tukisoma kutoka kwa Yoshua 1:

> *…baada ya kufa kwake Musa, mtumishi wa Bwana, Bwana akamwambia Yoshua, mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa, akasema,*
>
> *Musa mtumishi wangu amekufa; haya basi, ondoka, vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi niwapayo wana wa Israeli.*
>
> *Kila mahali zitakapopakanyaga nyayo za miguu yenu, nimewapa ninyi, kama nilivyomwapia Musa.*
>
> *Tangu jangwa hili na mlima huu, Lebanoni, mpaka mto ule mkubwa, mto wa Frati, nchi yote ya Wahiti, …tena mpaka bahari ile kubwa upande wa machweo ya jua, hapo ndipo patakapokuwa mpaka wenu.*
>
> *Hapatakuwa mtu ye yote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe; sitakupungukia wala sitakuacha.*
>
> *Uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa nchi hii niliyowaapia baba zao ya kwamba nitawapa.*
>
> *Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda sawasawa na sheria yote aliyokuamuru Musa mtumishi wangu; usiiache, kwenda mkono wa kuume, au wa kushoto, upate kufanikiwa sana kila uendako.*
>
> *Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana.*
>
> *Je! Si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako.*

8 Katika aya ya tano, na karibia katika ya hiyo aya, imeandikwa: *"Kama Nilivyokuwa Pamoja Na Musa, Ndivyo Nitakavyokuwa Pamoja Na Wewe*;" Hilo ndilo, kama ningeliita hilo somo, ningependa kusubiri kwa kitambo kidogo, na kunipa usikivu wenu kwenye hilo. "Kama Nilivyokuwa Pamoja Na Musa, Ndivyo Nitakavyokuwa Pamoja Na Wewe."

Sasa jioni iliyopita tulikuwa tukisafiri pamoja na wana wa Israeli kote kutokea Misri hadi tukawafikisha katika Kadeshi. Ee, lilikuwa somo kuu iliyoje! Ni jambo kuu iliyoje, tulivyolinganisha kanisa la kimwili na lile kanisa la kiroho: Mungu akishughulika na Israeli kimwili; pamoja na kanisa katika hizi siku, kama Yeye anavyoita watu watoke kwenye Mataifa kwa ajili ya jina Lake. Yeye anashughulika nao kiroho, kama alivyoshughulika nao kimwili. Ni usambamba tu, moja kwa hilo linguine. Yote yale Mungu alifanya na wao, na yote Mungu aliyofanya kwa ajili yao, na yote waliyofanya kama mwitikio, yanaangukia kwetu kama mfano. Na tunaona, hadi hapo, Neno limekuwa likitekelezwa vivyo hivyo kabisa: jinsi hilo katika mwili walipopata ushindi wao mmoja au mara mbili, walikaa na kufurahi, na kupiga kelele, na kucheza, na kumsifu Mungu, kama tu kanisa lilivyofanya; na sasa limesubiri kwa miaka arobaini kwa ajili ya kufunguliwa kwa kitu fulani kingine.

9 Na tunapomwazia Musa, huyu mtumishi mkuu wa Bwana, jinsi ambavyo katika kuzaliwa kwake, pale mahali alikozaliwa, Mungu alimchagua kwa ajili ya kazi yake, penye kuzaliwa kwake. Na maisha yake yalikuwa magumu kuyaishi kwa sababu yeye ni mwanadamu, na yeye anataka kuishi kwa namna moja, na Roho wa Mungu anamwongoza namna nyingine. Ni uamuzi wa kipumbavu iliyoje, ionekanavyo, kwamba yeye angefanya, wakati, akiwa na mguu kwenye kii cha enzi kuwa mrithi wa ulimwengu, na kisha

kuchukua ule upande mwingine na kuwa mgeni, au mwenye kutangatanga. Ionekanavyo, kiakili, ingekuwa kitu cha kipumbavu.

Lakini tunapata somo kuu hapa, kwamba watu wanaomfuata Roho ni upumbavu kwa ulimwengu, kwa sababu wao ni wa ufalme mwingine, wanaongozwa kwa namna nyingine, wanaongozwa na Roho. Mungu, hebu huyo awe mimi, na ninyi nyote, kwamba tutafuata uongozi wa Roho, iwe iwavyo, tukitazama ahadi ya Mungu, tukingojea itimizwe.

10 Na hilo ndilo tu Musa alilofanya. Farao alisoma maandiko yale yale Musa aliyosoma, ni kwamba tu Farao aliyaangalia kwa njia nyingine. Musa aliwaangalia watu wale wale ambao Farao aliwaangalia. Farao aliwaona kama watuma na wakanyaga matope; Musa aliwaona kama waliotwa na waliochaguliwa.

Hivyo ndivyo ninavyotaka kuliona kanisa la Mungu aliye hai. Siyo kundi la walokole wenye itikali kali au waliotengwa, bali kama waliochaguliwa na Mungu, ili niweze kuyatoa maisha yangu, kama Musa alivyofanya, kwa ajili ya hili kanisa kuu na kwa sababu hiyo.

Sasa tunamwona Musa akiwa ameitwa. Na baada ya kuwa ameagizwa, alishindwa agizo lake kwa kujaribu kulifanya kwa njia aliyofikiri ilikuwa bora.

Kwa hiyo hilo linatufundisha tena kwamba hatuwezi kuchukua kile tunachofikiria kuwa bora, au kile mwanadamu anachofikiria kuwa ni bora. Tunapaswa kuchukua ile njia ambayo Mungu amesema ni bora zaidi. Kwa hiyo, kufuata Neno la Bwana ni bora kabisa wakati wote. Chukua ile njia aliyoisema Mungu.

11 Na katika kushindwa kwake, tunaona kuwa alikimbia mbali na uso wa Farao kwenda jangwani, ambako alimwoa binti wa Yethro Zipora. Na baada ya kumwoa, alimzalia mwana, Gershomu. Kisha akatulia, kimya na kwa amani, alipokuwa katika kazi ya kondoo.

Lakini siku moja Mungu alisikia kilio cha watu Wake. Mungu alikumbuka kwamba alikuwa na agano na hao watu. Siyo hilo tu, lakini alikumbuka pia kwamba alikuwa na mtumishi ambaye alikuwa amemwita na kumchagua, na alikuwa na agano na huyo mtumishi. Na Mungu kamwe hatabadilisha agano Lake, au kubadilisha shauku Zake, au kubadilisha kitu chochote. Mungu wakati wote atatimiza ahadi Zake. Ijapokuwa Musa alikuwa amemkosea na alikuwa amefanya jambo ambalo lilikuwa makosa, bado Mungu alitimiza agano Lake. Wakati Mungu anapomwita mtu ili afanye kitu fulani, ni lazima akifanye, inampasa tu akifanye.

12 Mtu fulani aliniuliza wakati fulani uliopita, "Tutafute vipawa vyetu sasa kwa ajili ya huduma zetu?" Ndugu fulani wa Kimethodisti ambaye alikuwa ndio tu amempokea Roho Mtakatifu.

Nikasema, "Hapana, usifanye hivyo. Ukifanya, basi Mungu hawezi kukutumia." Nikasema, "Kitu pekee cha kufanya ni kuendelea tu kuwa Mkristo. Kama Mungu amekuita, Yeye atakuweka tu kabisa pale unapopaswa kuwa."

Mara nyingi, hao wanaotafuta na kujaribu kupata vitu, kama Mungu atawapa kitu fulani, sanasana wangejivuna. Kwa kawaida, mtu ambaye Mungu amemwita ndiye mtu ambaye anajaribu kumkimbia Yeyey, ikiwa chochote—Musa na Paulo, na wengine mbalimbali, wakijaribu kuwa mbali na huo mwito.

13 Lakini tunaona hapa kwamba Mungu, pamoja na kushindwa kote ambako Musa alifanya, bado Yeye alikuwa na mkono wake juu yake. Na alimwita kwenda kufanya huduma Yake, alimwita kwenye agizo lake. Na ni faraja iliyoje ambayo ingekuwa kwa Joshua wakati alipomsikia Mungu akisema, "Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe."

Ijapokuwa kama ninajaribu na nikashindwa, Mungu hataniacha. Kamwe sikuwa na ujasiri katika mtu yeyote anayeogopa sana kufanya kitu chochote. Ni bora nionekane mwenye kushindwa kuliko kuwa mvivu sana wa kujaribu.

14 Wakati mmoja ilisemwa kwamba ile Kampuni ya Ballard Flour ilimwajiri mtu, na alikuwa anaenda kusaini jina lake; na huyo mtu hakuwa na kifutio mwishoni mwa kalamu yake ya risasi. Na Bw. Ballard akamwambia, kasema, "Kwa nini huna kifutio?"

Akasema, "Huwa sifanyi makosa."

Akasema, "Basi siwezi kukutumia. Kwa sababu kama ukifanya makosa … usipofanya makosa, hutaweza kufanya chochote." Hilo ni kweli.

Mungu hakuwajibishi kwa makosa yako. Yeye hukuwajibisha kwa dhambi zako za makusudi. "Yeye afanyaye dhambi kwa kusudi baada ya kuwa amepokea ujuzi wa ile kweli…." Lakini mtu ambaye anaenda kufanya kitu fulani aatakosea, anaenda kuanguka. Yeye atafanya makosa. Lakini kama hakika ameitwa kiungu, na Mungu yuko moyoni mwake, atainuka tena.

15 Nilizoea kuwa, nikiwa nakuja kanisani hapa miaka iliyopita (na wao huenda wapo hapa asubuhi hii),

mtu mdogo na mke wake. Walizoea kuimba wimbo ambao ulinisisimua, ulikuwa kitu fulani kama hiki:

> Nisemehe, Bwana, na unijaribu mara moja
> zaidi,
> Nitakuwa wako kama utakuwa wangu;
> Kama nikianguka au kama nikishindwa, hebu
> niinuke nijaribu tena,
> Nisamehe, Bwana, na nijaribu mara moja
> zaidi.

Ninapenda hilo, kwa askari yeyote mzuri anastahili kujeruiwa au kuumizwa. Lakini kama bado ni askari, na ana kusudi na kitu fulani cha kupigania, atainuka na kujaribu tena. Askari yeyote mzuro wa msalaba atafanya kitu hicho hicho.

16 Na kwa Yoshua, kamanda mpya wa jeshi baada ya Musa kuwa amekufa, kule kuona kuwa Mungu alikaa naye katika makosa yake, alishikilia agizo lake ha-…

Haijalishi Musa alifanya nini, ilikuwa ni ofisi ya Musa ambayo Mungu aliiheshimu. Yeye alikuwa nabii. Alikuwa juu ya manabii wote. Hakika yeye alikuwa zaidi ya nabii yeyote ambaye waliwahi kuwa naye. Wakati dada yake mwenyewe alipomcheka kwa kuoa msichana Mkushi, Mungu aliwaita pamoja na kusema, "Hummwogopi Mungu?" Akasmea, "Kama akiwepo mmoja miongoni mwenu ambaye ni wa kiroho au nabii, nitanena naye katika maono na kujitambulisha mwenyewe kwake katika ndoto. Lakini sivyo hivyo kwa Musa. Ninanena mdogo kwa sikio na yeye. Hummwogopi Mungu?"

Ona, hilo siyo jambo jema, kuwakanyaga watu wa Mungu. Unamwuumiza Yeye unapofanya hivyo. Mungu alikuwa amemwagiza Musa. Kushindwa kwake hakukumaanisha chochote—Mungu aliujua moyo wake.

17 Na wakati mmoja Musa alilalamika kuwa na kazi nyingi za kufanya. Na hivyo Mungu akachukua Roho Wake na kumgawa miongoni mwa sabini. Hawakuwa na Roho zaidi kuliko waliyekuwa naye mwanzoni, lakini, kitu pekee, walikuwa tu na mtambo zaidi. Kiwango kile kile cha Roho.

Mungu anaweza kumweka Roho Wake juu ya mwanadamu kama akitaka, au Yeye anaweza kumgawanya miongoni mwa maelefu kama akitaka. Siku mmoja aliweka Roho Yake yote juu ya mtu mmoja aitwaye Yesu; sasa Yeye amemgawanya kupitia makanisa Yake kila mahali. Mungu hutimiza agizo Lake.

18 Sasa Yoshua, askari mpya. Wawili tu wamebakia sasa ambao waliondoka nchi ya ahadi. Hao walikuwa Yoshua na Kalebu. Sasa Yoshua kamanda mpya wa kuongoza jeshi, ili kuchukua mahali ambapo mtu mkuu kama Musa alisimama, haikuwa kazi ndogo.

Ninamfikiria mhudumu leo aliyeitwa na Mungu kutembea kwenye njia aliyosimama Yesu—ni amri iliyoje, ni agizo la jinsi gani. Lakini kila aliyeitwa nan Mungu ameagizwa kusimama mahali pale pale. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa njia." Kila mhudumu ameitwa asimame mahali Yeye alikosimama: "Kazi nizifanyazo nanyi mtazifanya pia." Kila mhudumu aliyechaguliwa na Mungu ameamrishwa kusimama katika njia za Yesu Kristo na kutekeleza wajibu ambao Yesu alitekeleza. Hilo ni amri kamili!

19 Na jinsi ambavyo hali ilikuwa wakati ambapo Yoshua, akiwa amesimama pale asubuhi ile akizungumza na Mungu, Yeye alisema, "Sitakuacha; na kama nilivyokuwa na Musa, hivyo nitakuwa pamoja nawe; hakuna mtu atakayesimama mbele yako katika siku zote za maisha yako. Nitaharibu na kugawanya. Nitaifanya njia iwe wazi, uwe tu hodari na ushujaa mwingi. Usifadhaike [hilo ni kuogpa]. Usiogope, niko pamoja nawe! Nitakuvusha." Ni agizo la jinsi gani kutolewa kwa huyu mtu mgeni aliyeitwa Yoshua.

Sasa, kuna mifano mikuu mingi hapa ambayo tungeweza kuiangalia, lakini tutairuka baadhi yake. Kwa mfano, kama Musa alikuwa kipindi cha kanisa ambacho kiliwaleta hadi Sinai, kwenye theolojia yao (ya usiku uliopita). Musa hakuruhusiwa kuwapeleka wana wa Israeli kule katika nchi ya ahadi kwa sababu alikuwa ameshindwa.

20 Na mashirika ya kanisa, madhehebu, yameshindwa. Hayatalipeleka kanisa kule! Mungu atainua mfumo mpya, mfumo usio wa kidhehebu, kwa nguvu ya Mungu, huo utalipeleka kanisa katika nchi ya ahadi. Mashirika na madhehebu yameharibu, kila moja likiendea theolojia yao wenyewe, kila moja likiendea njia yao wenyewe ya kufikiri. Lakini Mungu atamchukua Roho Wake Mtakatifu, na atawainua akina Yoshua Wake, ambao watalipeleka kanisa kwenye ahadi, bila ya masharti ya kidhehebu yakiwa yamefungwa kokote, lakini watalifikisha kanisa Lake kule.

Musa alikuwa ameshindwa. Yeye alikuwa mtoa sheria. Yoshua aliitwa kwa ajili ya neema, na alipeleka kanisa mbele.

21 Tunaona pia kwamba Yoshua, akijua hili agizo, akijua liko mikononi mwake, kwamba Mungu alikuwa

amemwita kwa ajili ya kazi ambayo hakupaswa kushindwa, alitembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu. Na alipowaita watu pamoja na kuwaambia kuwa Mungu alikuwa amemwagiza, tazama ombi la wale watu. Walisema, "Tutakufuata kama tulivyomfuata Musa kama tutaweza kuona kitu kile kile kilichomfuata Musa kikikufuata. Kuwa tu hodari na shujaa."

Hilo linapaswa kuwa hitaji la kila mtu aliyezaliwa mara ya pili leo. Kama tumeombwa kufuata, basi hebu tuone ishara zikimfuata mwammini. Kama Yesu alivyosema, "Mambo niyafanyao nanyi mtayafanya pia."

Na nimewaomba kabla kuwa na hakika kuruhusu moyo wako wa kiroho asubuhi hii, kwa sababu ninaamini mtalishika lile ninalosema. Kuketi na watu wa kidhehebu, aina zote za mashirika ya dini yamekusanyika hapo asubuhi hii, kutoka Katoliki na Pentekoste na aina nyingi mbalimbali, hivyo litafunuliwa kwa aliyejazwa Roho, bila shaka.

22 Sasa, ilimpasa Yoshua kuchukua hii amri. Watu walisema, "Hebu Mungu awe pamoja nawe kama Yeye alivyokuwa na Musa, na tutajua kwamba Roho yule yule ambaye alituongoza umbali huu anaweza kutupeleka mbele."

Loo, jinsi kanisa linavyopaswa kuonekana asubuhi hii kumwona Roho akifanya kazi miongoni mwa watu, kama unataka kanisa la nyumbani ambapo Roho alimfufua Kristo toka kwa wafu, Roho Mtakatifu, ambaye atatembea miongoni mwa watu. Huyo ni Roho ambaye Mungu anamwinua katika siku za mwisho kuwapeleka watu kule katika nchi nyingine, katika ahadi kamili ya baraka zote za Mungu, na kwenye agizo lote ambalo Yeye alitoa, au ile ahadi. "Ahadi ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu." Kama Israeli walivyotafuta ile nchi ya ahadi, wakijua kwamba ilikuwa mahali fulani kwa sababu huko paliwahi kuwepo mtu huko nyuma, vivyo hivyo na kanisa! Tunajua kuwa kuna nchi mahali fulani! Kuna nguvu mahali fulani kwa sababu kulikuwepo na wengine huko. Tunajua hiyo nchi iko ng'ambo ya mto, mahali tunakoelekea asubuhi hii, tukijaribu kwenda katika hiyo nchi ya ahadi.

Yoshua alijua kwamba ile nchi ilikuwa kule. Alikwenda kwanza na kuona, kisha angeweza kurudi kama shahidi.

Wahudumu walioitwa na Mungu hawapaswi kufungiwa na theolojia, lakini wameitembelea ile nchi kule tunakokwenda, wakileta ushahidi wa upendo wa Kiungu na nguvu za Yesu Kristo kufanya zijulikane kwenye makusanyiko yao kwamba kuna nchi ng'ambo ya mto.

23 Sasa, usiku uliopita nikihubiri kwenda hadi Yordani. Sasa, wakati tunapofika kwenye ule mto, huo unatugawa. Unatutenganisha. Mara unapokuwa upande ule mwingine, kitu fulani kimekutokea.

Sasa, Yoshua, katika hili lote, akijua kuwa hilo agizo lilikuwa kuu; lakini akiwa na uhakika, angeweza kutokuogopa, angeweza kuwa, kama ambavyo tungeliita hilo, asiyejali hatari—maadam alikuwa ameelekezwa njia sahihi. Angeweza kukutana na kilima ambacho kingemgonga na kumrudisha nyuma, lakini alikuwa anaeleke njia sahihi.

Na kanisa la Mungu aliye hai linaweza kuwa lisiloogopa hatari na lisilo na hofu katika imani kama tumeelekezwa njia sahihi; kwani Yeye alisema, "Kama nilivyokuwa na Musa, nitakuwa pamoja na wewe. Sitakupungukia wala sitakuacha." Yeye kamwe hakumwacha Musa. Yeye kamwe hakumpungukia Musa. Yeye hatampungukia Yoshua. Yeye hatatupungukia! Yeye atakuwa pamoja nasi.

24 Na kama tunavyomwona Yoshua akichukua hili agizo, akijua majukumu, alikuwa akiwaongoza kupitia nchi sasa ambazo … ingelimpasa kwenda kule katika ile nchi nyingine. Ingelimpasa kupangilia ufalme wao. Yeye angepaswa kugawanya urithi miongoni mwao. Alijua hilo agizo lilikuwa kuu, zaidi sana kuliko kile Musa alichokuwa amefanya. Yoshua alikuwa na mengi zaidi ya kufanya kuliko aliyokuwa amefanya Musa.

Jambo lingine, alikuwa awaongoze pale mpakani, miongoni mwa ndugu zao. Wao walikuwa wamekwishaonja ndamu. Alipaswa awashinde, alipaswa awanyamazishe, walipokuwa wakitembea.

Ndivyo ilivyo leo na hili kundi jipya la Kipentekoste linaloinuka sasa. Wao wameonja udhehebu. Ni vigumu sana kuwatuliza.

25 Miaka kadhaa iliyopita walisema, "Njoo, Ndugu Branhama [wakati huduma ilipoanza mara ya kwanza], tutaanzisha dhehebu, tukujengee kumbukumbu mahali fulani." Mimi sitafuti kumbukumbu! Ninatazamia Kuja kwa Bwana!

Waliunda dhehebu dogo lililoitwa "Mvua Ya Masika," wakaenda Canada na katika Calfornia; lakini lilishindwa. Bila shaka, lisingeweza kwenda. Kwa nini ilikuwa hivyo? Kitu pekee wanachojua…. Walitoka kwenye hivyo vitu, na walikuwa na mguso mdogo wa hicho. Walipaswa kuwa na kitu fulani walichopaswa kufanya.

Lakini, ndugu, kanisa halisi la Mungu aliye hai halina miundo, halina kanuni za imani. Linaongozwa na nguvu za Mungu aliye ndani ya moyo wa kila mmoja. Wapitie ndugu zako. Usigombane nao. Sisi ni wakuu

kuliko wao. Usigombane nao; pita tu pale.

26 Nawataka mwone, jambo kuu lililotokea hapa. Kulikuwa na Esau, Moabu, na wale tuliowazungumzia usiku uliopita. Wengi wa hao watu, wengi wa hao, kwa kweli walikuwa waamini wa mpakani. Walikuwa pale pale mpakani.

Loo, napaswa kusimama hapa juu ya jambo fulani kwa kitambo tu, haitachukua zaidi ya dakika moja. Watu wengi huchukulia ile nchi ya ahadi na Milenia. Siyo. Nchi ya ahadi ilikuwa na vita na mauaji; Milenia haitakuwa na vita vyovyote wala mauaji. Inaelekeza kwa Roho Mtakatifu, uwanja wa vita.

Kuhesabiwa haki, waliondoka Misri. Kuna hatua tatu za safari yao. Waliondoka Misri chini ya kuhesabiwa haki, wakiliamini Neno. Walijitenga wenyewe mbali na Wamisri na kutoka. Walivuka Bahari ya Shamu na kuua hayo mambo nyuma yao, ambapo ilikuwa ni utakaso, kupitia damu ambayo huua shauku zote za uovu za mwanadamu-hatua ya pili ya safari. Lakini ile hatua ya tatu ilikuwa walipovuka Yordani kuingia nchi ya ahadi ambako urithi wao ulikaa. Urithi wao kamwe haukukaa Misri, ingawa Mungu aliwabariki katika Misri.

27 Ninyi Walutheri mnaoamini katika kuhesabiwa haki, urithi wenu haukai hapo, kama mmeitwa. Kama wewe ni Mlutheri tu, huo ndio umbali wote ambao utaweza kufika.

Ninyi Wamethodisti, na Wanazarethi, na Pilgrim Holiness, na Church of God, mnaoamini katika utakaso, kule kuua uovu ulioko ndani yenu, kuondolea nje mizizi ya uovu, ninyi ni wa ng'ambo ya mto.

Lakini kwenu wanaume na wanawake ambao kuna kitu ndani yenu kinawaita mtoke, kilindi kwa kilindi, bado kuna Yordani ya kuvuka! Na nchi ng'ambo ya mto.

Akasema, "Mnakwenda kupita karibu na ndugu zenu. Mnakwenda kupita karibu na ndugu zenu, nao wako karibu na mpaka. Na kama mkipita karibu nao, msiwaambie chochote. Nimempa Esau huu mlima. Nimewapa Moabu hii nchi. Na sitaki mbishane nao, kuwaongoa. Mpite tu kiungwana. Mnajua kule mnakokwenda. Msichukue tabia zao."

28 Wamoabu walikuwa na nabii wa uongo, askofu kwa jina la Balaamu, aliyekuja na kuwa miongoni mwa kusanyiko ili kujaribu kuwafanya kuwa dhehebu na wote wakae pamoja, kwa sababu wao walikuwa ndugu. Lakini hawakuwa ndugu! Walikuwa ndugu nusu, siyo ndugu halisi! Kama moyoni mwako….

"Msipingane naye; endeleeni tu, mwacheni. Walipeni kwa kile mnachopata, kama mtapaswa kupitia katika nchi yake." Yeye aliwekewa kimbele kuwa hivyo. Kama Mungu angekuwa ametarajia au kuwachagua kimbele Wamoabu kuungana na Israeli, wangeliungana nao. Kama Yeye alimchagua Esau kimbele kwenda pamoja na Israeli, Esau angelirukia ndani na kwenda. Lakini Yeye alimpa urithi wake ng'ambo ile nyingine ya mto.

29 Vema, unawezaji kujaribu kuwafanya Walutheri wote walione jambo hilo, Wabaptisti wote walione jambo hilo, Wapresbiteria wote, na Wanazarethi, na Pilgrim Holiness? Usiwahukumu. Hilo ndiyo pekee wanalolijua. Ni hilo pekee lililoko ndani yao.

Lakini kwenu ninyi mnaoamini (Ee Mungu), kwenu ninyi mnaojua, kwenu ninyi mlio na kitu fulani ndani yenu ambacho kinaita kilindi! Kama kilindi chote mlicho nacho kimetoshelezwa, basi dumu pale ulipo. Lakini mimi na nyumba yangu, kwangu mimi, kuna kitu fulani zaidi kuliko kile yeye anachokiona! Kuna nchi ng'ambo ya mto mahali fulani, bado kuna kilindi kikiita kilindi. Siwezi kutoshelezwa na theolojia. Siwezi kutoshelezwa na kanisa zuri. Siwezi kutoshelezwa na kampeni nzuri. Siwezi kutoshelezwa na ibada ndogo ya uponyaji. Kuna kitu fulani zaidi ya hicho ambacho kinaita!

30 Hivyo waache tu. Nende moja kwa moja. Msibishane nao. Lakini tunapita kwenda nchi nyingine. Wao hawakuwekewa kwenda pamoja nanyi. Hawatatembea pamoja nanyi. Wawili wanawezaje kutembea isipokuwa wamekubalina? Lakini kwa hao wampendao Mungu, kwa hao walioitwa na Mungu…

Vema, wanasema, "Mungu alitupa kanisa. Mungu alifanya hili."

Hilo ni sahihi. Mungu kasema. "Nilimpa Esau mlima huu; usimguse. Lakini ninacho kitu fulani tofauti kwa ajili yako. Vuka kule!" Amina.

Hiyo ndiyo shauku yangu, ndugu, kuona kanisa langu likivuka kule kuingia nchi nyingine, shauku ya kwenda kule upande mwingine. Kama kuna kitu fulani ndani yako hapa kwanza, kikiita, kutakuwa na kitu fulani cha kuitikia huo mwito. Kuridhika tu na kuchunga kondoo halikutoshi, kwenda katika aina fulani ya kazi halikutoshi, kujiunga tu na kanisa na kuandika jina lako kwenye kitabu halikutoshi; kwa sababu kuna kitu fulani kinaita, kote kuvuka kilima kule, kuvuka kilima kinachofuata, na kote kuvuka Yordani, hadi uangukie mikononi mwa Mungu kule. Kilindi kikiika kilindi.

31 Yoshua alijua hili agizo lilikuwa kuu. Uliona wakati Yoshua alipoanza kuvuka Yordani jinsi Yoshua alivyokumbuka agizo lake? "Hebu Kitabu hiki cha torati [Neno Langu] kisiondoke kinywani mwako." Kwa

maneno mengine, "Yoshua, sijali kabila linasema nini, ni nini huyo kiongozi wa kidini mwingine anasema, dumu na hili Neno! kisha ndipo utafanya njia zako zistawi. Haijalishi ni mambo mangapi makubwa wanafanya, na mambo mangapi madogo wanafanya, na ni madhehebu mangapi wanaunda, dumu na Neno, Yoshua! [Loo, jamani!] Dumu na Neno. Hili Neno lisiondoke kinywani mwako…." Hebu nilisome tena:

*Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda sawasawa na sheria yote aliyokuamuru Musa mtumishi wangu; usiiache, kwenda mkono wa kuume, au wa kushoto.*

32 Kama Neno linasema fanya jambo fulani, lifanye! Mimi sijali kile dhehebu linasema, lifanya hata hivyo! Huyo ndiye Yoshua ambaye Mungu anamsubiri. Usigeuke inchi moja, yodi moja. Dumu moja kwa moja na Neno.

*… usiiache kwenda kulia … au kushoto, upate kufanikiwa.*

Loo, mnafikiri mnafanikiwa wakati mnapojenga makanisa makubwa, kupata washirika elfu kumi walioongezeka kwenye dhehebu lenu. Hayo siyo mafanikio. Hilo halikupeleki hatua moja karibu zaidi na ile ahadi. Kile tunachohitaji ni Mungu zaidi, Roho Mtakatifu zaidi!

*…upate kufanikiwa popote uendapo.*

*Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako; bali yatafakari maneno yake mchana na usiku.*

Wakati unapofikiria kufanya jambo fulani, unalichukua Neno la Mungu kwa ajili jambo hilo? Je, unatafuta shauku yako katika Neno? Je, unahubiri kile ambacho ni Biblia? Au upo tu kama wengi leo, na wengi mno, "wakiubiri kwa ajili ya mafundisho yaliyo amri za wanadamu?"

33 *Kitabu hiki cha torati kisiondoke mkononi mwako … au, kinywani mwako.*

"Kinywani mwako," kile unachosema Usikisome tu na kuondoka. Kinene! Kiishi! Kifundishe!

*… bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo*

Unaona Yoshua wa siku ya leo anaenda kuwa nini? Ona kile Yoshua wa kanisa la kiroho anachokwenda kuwa? Ni aina ya Yoshua yule yule waliyekuwa naye kimwili, Kanisa la kiroho linapaswa kuwa kitu kile kile.

Kama Biblia ilisema, "Mtu asipozaliwa mara pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu," Yoshua wa kiroho atasema, "Amina."

Kama Biblia inasema, "Yesu Kristo ni Yeye Yule jana, leo, na hata milele na milele," Yoshua wa kiroho atasema kitu kile kile. Yeye ni yule yule.

Kama Biblia inasema, kile Kitabu, Lile Neno, husema kwamba, "Kaeni katika mji wa Yerusalemu hata mvikwe uwezo utokao juu. Baada ya hapo Roho Mtakatifu atawajilia, kisha mtakuwa mashahidi wangu," Yoshua wa kiroho anasema kitu kile kile.

34 Kama Petro, penye siku ya Pentekoste, alisema, "Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika jina Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu, mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu," Yoshua wa kiroho hataondoa yodi moja kamwe, lakini atakuwa kile Neno linachosema kabisa.

Kama Marko 16 inasema, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa. Na ishara hizi zitawafuata hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru; kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya," Yoshua wa Kiroho atasema kitu kile kile. Atayatafakari hayo mchana na usiku, kufanya hiyo njia kuwa ya mafanikio.

35 Nawataka mwone ni nini kilitukia. Yoshua, wakati alipokuja kwenye kampeni yake ya kwanza, mara ya kwanza kuthibitisha kwamba alikuwa Yoshua halisi…. Israeli ilipaswa wawe walijua hilo.

Hapana shaka viongozi wa kanisa walikuwa na wazo tofauti. Walisema, "Sasa tutaweka kambi hapa hadi wakati wa kuchipua … au, hadi wakati wa kiangazi, Yordani itapungua."

Huonekana kama kwamba Mungu hutupia baadhi ya vitu vya kijinga zaidi mbele ya akina Yoshua wa kiroho.

Alimleta pale mnamo mwezi wa Aprili, wakati Yordani ulikuwa mara tatu au nne ya ukubwa wake. Alikuwa akimjaribu, kuona kama alikuwa Yoshua hasa.

Hebu kila kikae vibaya, hebu kila mtu mwingine afanikiwe, hebu makosa yastawi. Hebu watu wenye mfano wa utauwa, wakane nguvu Zake, wafanikiwe, na kukusukuma nyuma. Lakini kama unajua pale

ulikosimama, utasimama! Haijalishi, kama ulimwengu wote unakuacha, utasimama hata hivyo. Hutaondoka kwenye hilo Neno.

36 Yordani ilikuwa mara tatu au nne zaidi ya ukubwa wake, wa kutisha, ulionekana wakutisha, wenye tope. Lakini Yoshua kasema, "Mungu alisema ndani ya siku tatu tutakwenda kule. Na tunakwenda kule!"

Sasa makasisi wanasema, "Sasa dakika moja tu, Yoshua. Sisi ni watu wasomi. Sisi ni werevu. Wengi wetu hapa ni wahandisi kutoka Misri. Tunajua namna kufanya haya mambo, hivyo tutasubiri tu kwa kitambo kidogo hadi mto uwe safi na tutaweza kutembea tuvuke. He, hilo siyo rahisi zaidi?"

"Sijali unafikiria nini. Mungu alisema siku tatu tunakwenda kule, na tunakwenda kule! Tunakwenda kule ndani ya siku tatu."

Tazama kile Yoshua alichofanya. Ni nini aliweka kuwa cha kwanza? Makasisi? Hapana, bwana. Alitanguliza Neno. Kasema, "Chukua lile sanduku la agano! Na ninyi makuhani kaeni mbali nalo. Kaeni nyuma yake. Msijaribu kuliongoza; liacheni liwaongoze."

37 Hilo ndilo tatizo leo. Tunajaribu kuwa mbele ya Neno, na kulikwepa, na kufanya Neno lilingane hiki, na Neno lilingane na kile. Ibarikiwe mioyo yenu, tunachohitaji leo ni, kufuata Neno!

Neno liliongoza njia. Wakati lilipofika Yordani ulifunguka, nao wakaenda kule. Katika kampeni yake ya kwanza, aliweka vitu view vya kwanza. Alikuwa na sababu kwa ajili hilo. Alikuwa na sababu, kwa sababu Mungu alikuwa amemwagiza, "Dumu na Neno. Acha Neno lifanya." Kila kampeni, walienda vitani, kwa sababu Mungu alikuwa amemwajibisha, waliweka sanduku la agano la kwanza.

Baada ya sanduku la agano kupita mbele, kisha ni nini kilifuata? Kuimba, wapiga vyombo vya muzuki, kabla mapigano hayajatukia. Haleluya!

Hilo ndilo tunalohitaji leo, kile tulichokuwa nacho asubuhi hii: waimbaji, vyombo vya muziki, kupiga muziki, kushangilia. Kisha kuweka Neno kwanza, kusoma Neno. Kisha vita vinaanza. Tunakuwa na hakika ya kushinda, tunapaswa tu kushinda. Dumu moja kwa moja nalo, shikilia mwelekeo wake, na litakushikilia wakati wa shida.

38 Alikuwa na sababu nzuri kwa ajili ya hilo. Sasa kumbukeni, wakati alipovuka, kabla ya kvuka, alituma mpelelezi kule, wawili, kuichunguza ile nchi. Sasa, Musa alikuwa ametuma kundi lote kule, lakini wote walirudi wakiwa wamechanganyikiwa. Tazama ile huduma mpya. Kamwe hakufanya hivyo. Alijua unapokuwa na mawazo tofauti elfu moja na mia tano unapata machafuko elfu na mia tano. Lakini alituma wawili. Kasema, "Nendeni kule, ipelelezeni hiyo nchi."

Sasa tunataka kufikia jambo fulani ambalo sitaki mlikose. Yeye alisema, "Sasa wakati mtakapokwenda kule…." Walipita kule, ili kuitazama ile nchi, waone kama hizo ahadi zilikuwa sahihi, waone kama ilikuwa … ilikuwa nchi ya aina gani, na namna gani wangeingia. Wakavuka. Majina ya wale wapelelezi hayakutolewa. Lakini walipokwenda katika ile nchi walifikia Yeriko yenyewe. Na walipofika Yeriko, nini kilitokea? Walikutana na kahaba, mwanamke aliyekuwa na ushuhuda wa aibu.

39 Nataka kuchora picha. Labda siyo sahihi, lakini nataka kujenga hoja kwa kuitumia hiyo. Hatuna historia ya Rahabu. Tunajua kwamba yeye alikuwa kahaba. Hebu tuwazie alikuwa alilelewa katika nyumba ambayo walikuwa masikini hasa, na akawa na ushuhuda mbaya. Naye ni mwanamke kijana mrembo. Aiienda barabarani kuwatafutia mama na baba yake walemavu mahitaji; hakukuweko na namna ya yeye kufanya kazi, bali kuuza tu uadilifu wa mwili wake. Lakini naweza kuwazia wakati wote alijua hilo lilikuwa kosa. Kuna kitu fulani ndani yake kilichomwambia, "Siyo sahihi kufanya hivyo." Alijua haikuwa sahihi.

Siku moja alisikia kwamba kulikuwa na Mungu ambaye alikuwa anasafiri. Moyo wake ukaanza kutetemeka. Akawaona wajumbe kutoka kwenye hilo vuguvugu kuu, ambao walimwambia kile kinachokwenda kutokea. Alisema nini? Sasa Yoshua alikuwa na ishara. Yoshua alikuwa na ishara zile zile alizokuwa nazo Musa, kabisa. Hivyo yeye alipokuwa … Rahabu hakuomba kuona ishara ya Yoshua; alisikia tu.

Mfano wa kanisa, mfano wa kanisa la kweli ambalo limevutwa mbali na ukahaba. "Mimi ni Mmethodisti leo, Mbaptisti kesho, Mpresbiteria kesho kutwa." Lililovutiwa ndani ya ukahaba.

40 Lakini ghafla, mhubiri mdogo anaingia mjini na kusema, "Kuna Mungu aliye hai, aliye hai jana na ni yeye yule yule leo. Nguvu Zake ni zile zile. Hufanya matendo yale yale aliyoyafanya alipokuwa hapa duniani." Mawakala Wake wako njiani.

Sasa, Rahabu kahaba, alijulikana kama kahaba, alikuwa mfano wa mwamini leo, mwamini halisi. Hakusema, "Sasa nasikia kwamba Yoshua anaweza kufanya ishara kwa sababu yeye ni mrithi wa Musa. Ningependa kuona hizo ishara. Na kama ningeweza kuona hizo ishara, basi nitaliamini." Vema, yeye hakupaswa kuonyesha hizo ishara kabisa, kwa sababu Rahabu aliamini hata hivyo. Rahabu hakuwa Tomaso. Aliliamini hilo.

41 Sasa, Musa, alipokuwa na ishara, alikwenda kule na kufanya hizo ishara, lakini ishara siyo kile kitu ambacho kiliwapeleka kwenye nchi ya ahadi. Haikuwa hiyo. Ishara zilikuwa ni uthibitisho wa lile agizo.

Na Rahabu aliliamini hilo pasipo kuona kitu chochote! Alisema, "Wote tunatetemeka."

Si ajabu Nikodemu alisema, "Rabi, tunajua wewe ni mwalimu kutoka kwa Mungu: hakuna mtu anayeweza kufanya haya mambo, isipokuwa Mungu alikuwa pamoja naye. Wote tunajua hilo."

Ulimwengu unajua hilo leo! Billy Grahama anaita, "Tunapaswa kurejea Pentekoste." Baraza la makanisa linaita, Tunapaswa kurejea kwa manabii, kwa wanenaji wa lugha, kwa wafasiri wa lugha, kwenye uponyaji wa Kiungu, waponyaji katika makanisa yetu, waruhusu Roho wa Mungu awe na njia Yake sahihi." Mungu anatoa wito Wake. Watu wanaogopa utauwa halisi, na husema, "Kila kitu … mioyo yetu inazimia ndani yetu."

42 Sasa, Rahabu hakupaswa kuona ishara ambayo Yoshua angeweza kufanya kwa mkono wake au kwa fimbo. Aliamini. Akasema, "Nilisikia, na naamini, na sasa ninaomba rehema. [Loo, jinsi tungeweza kuweka somo hapa hapa!] Naomba rehema kwa ajili yangu na nyumba yangu."

Mtazame yule Mrumi, usiku ule, aliyevuta upanga wake na alikuwa anakwenda kujiua, yule msimamizi wa gereza la Filipi. Paulo alisema, "Usijidhuru mwenyewe. Wote tuko hapa."

Kasema, Nifanya nini niweze kuokoka?"

Kasema, "Mwamini Bwana Yesu Kristo; wewe na nyumba yako mtaokoka."

Kwa nini? "Wewe na nyumba yako"? Hakika. Nyumba yako itaokolewa pamoja na wewe. Kwa nini? Kama unayo imani kutosha kukufanya uokoke, unaweza kuwa na imani kwa jili ya familia yako kuokolewa. Ndiyo, wewe na nyumba yako!

43 Mtazame Rahabu. Rahabu alisema, "Nirehemu! Usiniue. Sitaki kufa pamoja na hawa wasioamini. Sitaki kufa kama mnyama! Nataka kufa katika mikono ya Yehova. Namwamini Mungu wenu, kwa sababu Yeye ni yote Mungu wa mbingu na nchi. Yeye hufanya mambo yanayoonekana. Yeye hufanya mambo kuwa halisi. Mimi sijawahi kumwona akifanya hilo, lakini naliamini hilo hata hivyo." Ona, kamwe hakuwahi kumwona Yoshua; alisikia tu juu ya Yoshua. Yeye hakuwahi kumwona Mungu, hakuwahi kuona lolote la matendo ya Mungu; alisikia tu. Wengine walikuwa meona hilo, naye akaamini kwa kulisikia. Sasa, kasema, "Ninataka mnisaidie, na baba yangu, mama yangu. Wote wawili ni wazee na walemavu. Ninao ndugu fulani. Nataka kuwa na imani kwa ajili yao."

Na wale wapelelezi, wahubiri, wakasema, "Ndiyo, yeye anakuja kupitia njia hii, na tunakwenda kuichukua nchi. Sasa, kama unataka wao waokolewe, waingize ndani ya nyumba. [Haleluya!] Kama unaamini hilo, nenda kawalete na uwaingize ndani hapa, kwa kuwa hatutawajibika kama watakuwa mitaani. Lakini kama tu utawaingiza ndani ya nyumba, tutawajibika [haleluya, pale ambapo uzi mwekundu ulikuwa unaning'inia dirishani]. Tutawajibika kama ukiwaweka ndani ya nyumba."

44 Loo, ndugu, kama paliwahi kuwepo na wakati tunapaswa kuwaingiza wapenzi wetu ndani ya nyumba, ni leo—nyumba ya imani. Waingize ndani, kwa kuwa wakati unakuja ambapo kutakuwa na mtikisiko. Baba zetu pekee, na akina mama, na akina ndugu, na akina dada wako salama ndani ya nyumba, kwa sababu nguvu za Mungu zinakwenda kuitikisa nchi tena. Ni hivyo. Na ni ile kaya ya imani pekee itakayookolewa.

Sasa yeye alisema, "Mimi siwajibiki isipokuwa umewaingiza ndani ya nyumba." Na Rahabu aliwafanya wajiapize kwamba wasingemwangamiza yeye au familia yake. Akasema, Kama utawaingiza ndani, watakuwa salama." Aliwashusha chini kuwaondoa mahali hapo, na wao wakaondoka.

45 Huyu kahaba mkuu, Rahabu, alifanyika mwamini. Nilisoma historia yake hapa muda siyo mrefu. Baada ya kufikiriwa kwa makini na kuletwa kwenye imani (kwa sababu ya imani yake kwa Mungu, aliletwa kwenye imani ya Kiisraeli, aliyeongoka), alichumbiana na jemedari katika jeshi, jeshi la Israeli. Tazama kile Mungu alichomfanyia yule mwanamke. Na walikuwa na ninii…. Walielekea Bethlehemu na wakapata mtoto wa kiume. Na huyo mwana, walimwita Boazi. Kutoka kwa Boazi … alimwoa Ruthi, kutoka kwa Ruthu na Boazi alitokea Yese; na kutoka kwa Yese alikuja Daudi; kutoka kwa Daudi anakuja Yesu. Haleluya!

Kwani nini? Imani huja kwa kusikia," kumsikia Mungu ambaye ni Mungu wa mbinguni na duniani, na kumwamini Yeye. Kuamini nini? Lile agizo ambalo Mungu ametoa kwa mwanadamu aliyeitwa Yoshua, akiamini hilo agizo.

46 Yoshua alikuwa na imani katika agizo lake mwenyewe, kama Musa alivyokuwa na imani. Mambo yalienda mrama kwa Musa, ilionekana kama kwamba alishindwa mara nyingi, lakini alipita kwa ushindi na kufia juu ya mwamba. Malaika wakamchukua.

Mungu, niache nienda namna hiyo. Hebu nishikilie agizo langu hadi siku fulani, nitakapokuwa tayari kufa, nitauona huo mwamba ukiwa umelala pembeni yangu.

Yoshua anatimiza agizo lake. Ijapokuwa alikuwa…. Mungu atalishikilia kitakatifu, kwa sababu alidumu moja kwa moja na Neno.

Sasa, Rahabu alijua kuwa Yoshua alikuwa na hili agizo. Sasa usilikose hilo. Shikilia hayo mambo moyoni mwako. Yoshua alikuwa na agizo. Rahabu alilitambua kabla ya kuona kitu chochote. Alijua Yoshua alikuwa na nguvu za Mungu ambazo zilikuwa zinaenda kuichukua nchi. Aliomba rehema. Mungu alimjalia rehema. Sasa wakati Yoshua alipokuja katika hiyo nchi, bila shaka tunajua, Rahabu alisalimika.

47 Lakini basi agizo lingine kuu Yoshua alilokuwa nalo lilikuwa kugawanya nchi kwa watu.

Sasa kumbukeni, "Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako." Hivyo alikuwa na Neno la Mungu. "Kama nilikuwa pamoja na Musa, endelea mbele moja kwa moja. Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe. Sitakupungia. Unaweza kunipungukia, lakini sitakupungukia. Lakini kama ukinikosea, Neema yangu yatosha, nitakuvumilia moja kwa moja. Endelea tu mbele. Maadam unadumu na Neno Langu, nitakutunza."

48 Sasa alipaswa kugawanya nchi, na kulikuwa na kabila kumi na mbili za kugawia hiyo nchi. Sasa vipi kama alikuwa na aliowapendelea? Vipi kama alipenda kabila la Gadi zaidi kuliko kabila la Efraimu, kabila Yusufu zaidi kuliko alivyolipenda la Yuda? Lakini hakufanya namna hiyo. Aligawanya kulingana na Neno, lililofunuliwa na Roho. Aliigawanya kulingana na kabila. Na angalia, alilifanya hilo kwa ufunuo, kwa utambuzi. Kwa utambuzi wa Roho wa Mungu, alilifanya hilo.

Kila mmoja wa hao akina mama wa Kihebrania, walipokuwa wakiwazaa hao Watoto, waliwataja majina yao. Na kila moja ya majina yao lilikuwa na maana.

Yakobo, alipozaliwa, akiwa pacha, mama alimwita "mlaghai." *Yakobo*. Lakini alipopata nguvu zake za kushinda, na kushikana mweleka na Malaika, Mungu alibadilisha jina lake kutoka Yakobo kuwa *Israeli*, "mwana wa mfalme."

Jina lina kitu fulani kinachohusiana na maisha yako. Wakati Petro, mvuvi, aliposhinda kwa imani yake katika Yesu, Yeye alisema, "Jina lako ni Simoni; lakini nitakuita *Petro*, ambalo ni "mwambo mdogo,.'" Linakubadilisha. Jina lako lina kitu fulani kinachohusiana nalo, na sehemu yako katika maisha.

49 Na wakati hili jambo kuu lilipotokea, wakati kila mmoja wa hawa akina mama wa Kiebrania, katika utungu wao katika kuzaa waliita, kama "Rubeni" hilo lilimweka mahali pake katika … Palestina, jinsi mama alivyosema kabisa na kuita jina lake, alivyolisema. Sina lote hilo llikiwa limeandikwa hapa, lakini *Rubeni* lilimaanisha "mchunga kondoo," *Gadi* linamaanisha "mfuga ng'ombe," na *Efraimu* lilimaanisha "mkulima wa mahindi."

Sasa, kwa utambuzi wa kiroho Yoshua, kiongozi mpya, kwa utambuzi wa kiroho, alimweka kila mmoja mahali pake, aligawanya hiyo nchi kwa usahihi kabisa.

50 Mfano mzuri sana leo, wa kwa nini tunamhitaji Yoshua leo. Shida leo, wakati tunapokuja katika nchi yetu ya ahadi, Gadi anataka kufuga kondoo kama Efraimu, mmoja nataka kufuga kitu fulani kama mwenzake. Kila mtu anataka kufanana na mwenzake. Hebu Mung ampe mtu mmoja karama ya uponyaji, kila mtu anataka karama ya uponyaji. Efraimu na Gadi na wote wanataka kujichanganya wote na kuwa kama mmoja. Lakini tumegawanywa katika nafasi zetu. Siyo wote wana karama ya hekima, siyo wote wana unabii, siyo wote wananena kwa lugha, siyo wote manabii. Lakini Mungu ameweka katika kanisa wengine watoa unabii, wengine wanaonena kwa lugha. Tunataka kuwafanya wote wanene kwa lugha. Unaona machafuko yalivyo? Basi hamwezi kwenda popote. Mbona, Wafilisti wangewapeleka huko kidogo. Hakika. Lakini wakati kila mtu, kwa njia ya kiongozi, alipowatenganisha kwa njia ya utambuzi wa roho na kuwaweka katika mwili, walibakia pale na kufanyika krimu ya dunia! Mungu, tupe Yoshua. Mungu, turejeshee Yoshua ambaye atashikilia hilo agizo pamoja na Neno.

Ndiyo sababu Mungu akamwambia, "Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku," kwa kuwa alikuwa na agizo mbele yake.

51 Sasa, Yoshua kiongozi mkuu alifanyika nini, kamwe hakushindwa vita isipokuwa kitu fulani kiwe kilikwenda vibaya kanisani. Wakati Akani alipochukua kabari, haikuwa sura ya Yoshua… au, imani iliyofanya jambo hilo. Haikuwa… Alichukua joho la Kibabeli na kabari ya dhahabu kutoka kambini; na alipofanya hivyo, hilo lilizorotesha vita yote.

Kiungo kimoja kinapoteseka, viungo vyote vinateseka. Mungu anajia nini mojawapo ya siku hizi, ndugu, ni kanisa lisilo na waa wala kunyanzi. Anakuja kwa kanisa lililojazwa Roho ambalo upendo wa Kiungu wa Mungu umeunganisha mioyo yao pamoja mno kiasi kwamba wanatembea kama mmoja.

52 Inapasa kushinda vita vya haya machafuko yote. Je, Methodisti liko sahihi, Baptisti liko sahihi, Presbitera, Pentekoste, Nazareti, Pilgrim Holiness? Madhehebu mia tisa na sitini na tisa tofauti, mbali na Wabudha na hizo aina nyingine zote. Tuko wapi? Kitu fulani kimeenda kombo. Kuna kabari kambini mahali

fulani. Yoshua apige kura.

Hebu na niseme hili asubuhi hii, kama Elia juu ya Mlima Karmeli, "Kama Mungu akiwa Mungu, hebu na ajibu kama Mungu." Kama dhehebu la Baptisti liko sahihi, hebu tuwaone wakitoa ishara za Yesu Kristo. Kama Nazareti liko sahihi, hebu tuwaone wakitoa ishara, wakifanya yale mambo Yeye aliyofanya. Kama Pentekoste liko sahihi, hebu tuwaone wakifanya kile kitu Yeye alichofanya. Kisha tutajua.

53 Wanafunzi wa Yoshua walisema, "Tutakufuata maadam tunamwona Mungu akitenda kazi pamoja na wewe kama alivyomfanyia Musa."

Na wanafunzi wa Yesu Kristo wanapaswa kusema jambo lile lile: "Tutatenda kazi na wewe tunapoona ishara za Yesu Kristo zikitenda kazi pamoja na wewe. Tutafanya hivyo." Hilo ndilo tunalopaswa kufanya, hilo ndilo kanisa linapaswa kusema. Huo ndio unaopaswa kuwa mtazamo wa Kanisa la Kikristo. Kisha ungeweza kuweka katika utaratibu karama, ishara, watenda kazi. Kama mtu mmoja ni mponyaji wa Kiungu, hilo halihusiani na yule ambaye anayenena kwa lugha. Yule anayenena kwa lugha hausiani karama ya unabii. Ona, tuna hatua tofauti za hii huduma.

54 Sasa, Mungu aliponipa utume wangu…. Nimeweka msingi lote hili kwa hili kusudi moja. "Karama na miito havina majuto." Hakuna mtu anayeweza kujifanya mwenyewe kuwa kitu chochote. Mungu ndiye anayekufanya kuwa kile ulicho, kwa neema Yake. Hatuna njia ya kujifanya wenyewe. Yesu alisema, "Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja?" Ni nani awezaye kujifanya mwenyewe mkubwa zaidi au mdogo zaidi kwa kuwaza? Huwezi kufanya hilo.

Mungu alipotoa agizo, nililihoji. Nikasema, "Mimi sifai … au sitoshelezi. Sina elimu. Siwezi kufanya haya mambo.

Na wengi wenu ninyi watu hapa asubuhi hii, bado mnaishi hapa leo … wakati Yeye alipotokea chini hapa mtoni, katika lile umbo la Nguzo ya Moto, na kusimama pale na kunena, na kusema, "Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kuwa mtangulizi wa Kuja kwa kwanza kwa Yesu Kristo, hivyo Ujumbe wako utatangulia Kuja kwa pili."

55 Tazama kile ilichofanya. Ile nuru ikining'inia pale, iliingia kwenye gazeti, ilienda kote katika Amerika na katika mataifa mengine.

Dr. Lee Vayle pale alikuwa Canada wakati huo. Anakumbuka wakati ilipotolewa katika gazeti la Canada, ninaamini ilitolwa. Sivyo, Lee Vayle? Katika gazeti la Canada, "Nuru ya ajabu yatokea juu ya kichwa cha mhudumu wa eneo la nyumbani alipokuwa akibatiza."

Watu wengi walisema, "Ni saikolojia."

Lakini siku moja Mungu aliamua kukomesha kinywa cha wasioamini, kwa sababu ilidumu na Neno. Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, ni ile ile leo hii, ikiongoza kanisa kiroho—ni ile ile kama ilivyoongoza kimwili. Yeye alionekana tena, na wakapiga picha mbele za wakosoaji, na mbele ya wachunguzi. Hii hapa inaning'inia sasa, ukweli usioshindwa, akifanya kazi zile zile, kuongoza watu kiroho kama ilivyowaongoza kimwili nyuma kule, ikidumu na Neno.

Sasa ulisema, Agizo lilikuwa ni nini?" Sasa kumbukeni, Mungu kamwe hawezi kuondoka kwenye agizo Lake.

56 Ningependa kuwachorea hilo, au kwa namna fulani. Tutalichukua hilo namna hii hapa. *Hii* hapa ishara ndogo, hilo ndilo agizo; sasa huu *hapa* ni msalaba mdogo katika kona moja, na Biblia kwenye kona nyingine, lakini maandishi yako katikati *hapa*. Hilo ndilo agizo.

Ninawachagiza mbele za Mungu, na malaika wateule, na Yesu Kristo. Lile agizo lilikuwa, "Ombea wagonjwa." Swali lilikuwa, "sitoshelezi kulifanya?"

"Ulizaliwa kwa kusudi hili, hii ndiyo sababu ya kuzaliwa kwako na maisha yasiyo ya kawaida, kwamba utaombea wagonjwa. Kama utawafanya wakuamini, na kuwa mwaminifu unapoomba, hakuna chochote kitakachosimama mbele ya maombi yako, hata kama ni saratani." Wangapi wamesoma hilo, kwa miaka kadha? Liko kote ulimwenguni.

57 Sasa, sasa nilisema, "Siwezi kulifanya hilo, kwa sababu sitoshelezi kulifanya hilo. Hawataniamini — mimi ni masikini, sina elimu." Huyo ni mimi nikihoji.

Yeye akasema, "Kama Musa alivyopewa ishara mbili ku-kuthbitisha agizo lake hivyo [siyo mapenzi yako]… unapewa ishara mbili. Mojawapo itakuwa kwa mkono wako. Hiyo nyingine itakuwa utajua siri za mioyo yao hasa, mawazo ya akili zao. Na kwa hili wataamini, kwa hizi ishara mbili." Sasa kumbukeni. Sikilizeni. Msikose kulipata hili. Ishara siyo agizo! Ishara inaelekeza tu kwenye agizo.

Unatoka nje hapa barabarani na unaona ishara, na inasema, "Maili tano hadi Jeffersonville," hiyo siyo

Jeffersonville. Hiyo ni ishara kukuonyesha uko kwenye barabara sahihi.

58 Vipi kama Musa, alipokwenda kule…? Yeye alikuwa na ishara, akiwa na fimbo na mkono wake. Ile ishara hapa siyo agizo zaidi kuliko ilivyokuwa kwa Musa. Vipi kama Waisiraeli wote wanasema, "Sema, ninyi Wamisri wote, Israeli wote, njooni hapa. Tunaye mtu anayeweza kufanya ujanja kwa mkono wake. Mnapaswa kuliona hilo. Tunaye mtu anayeweza kuchukua fimbo na kuigeuza kuwa nyoka. Njooni mwone"? Hiyo ilikuwa ni bango la ishara tu. Hilo halikuwa agizo. Wao hawakuwa wanasubiria bango la ishara. (Mungu tusaidie.) Wao walikuwa wanasubiri ukombozi!

Na huu ulimwengu masikini, mgonjwa, uliolemaa unasubiri ukombozi, na unaangalia kwenye bango la ishara. Turehemu! Bango la ishara siyo chochote ila ni alama kuthibitisha hilo agizo. Hiyo hapo huduma mpya. Imefunuliwa tu kwangu. "Ombea wagonjwa. Wafanye watu wakuamini." Mungu kamwe hawezi kuliacha hilo. Hilo ni agizo Lake, haidhuru nini kinaendelea, ninashindwa kiasi gani. Ninashindwa kiasi cha kusikitisha. Sikupaswa kamwe kuendelea na hizo ishara; hayo hayakuwa mapenzi ya Mungu, lakini Mungu amelibariki hata hivyo. Lakini niko tayari kuondoka kwenye huu mlima. Ninataka kwenda kuvuka Yordani. Ninataka kubeba hilo agizo. "Wafanye watu wakuamini."

Nikasema, "Hawataniamini."

"Kutaongezwa ishara mbili.

59 Sasa shida ya hilo ni kuwa tumekuwa tukiangalia kwenye ishara.

"Loo, Ndugu Branham, weka mkono wako juu yake."

"Loo, unapaswa kuona ni nini kinachotokea. Simama mbele yake wakati upako uko juu yake, atakuambia kila kitu kilichoko moyoni mwako." Hilo ni kweli.

Nilikwenda hospitalini hapa hivi majuzi. Kulikuwa na madaktari, hawakuweza kuona tatizo la huyo mwanamke. Madaktari walipoondoka chumbani bibiye Fulani akarudi, naye alikuwa akisimama kwenye hicho kitanda. "Wamesema hawawezi kuona chochote ambacho ni tatizo." Kasema, "Ndugu Branham, unaweza kuniambia!"

Nikasema, "Kama utaniamini, ninaweza."

Yule mwanamke akasema, "Ninaamini"

Na Roho Mtakatifu kasema, "Kitu hiki-na-hiki." Hicho ndicho hasa, kilicho. Ona kama siyo hicho." Yeye ni mshirika wa kusanyiko la Junie Cash.

60 Mwanamke mwingine pale alisema, "Mgongo wangu," kasema, "hawewizi kuona ni nini kilifanya hilo."

Nikasema, "Unaniamini mimi kuwa nabii Wake?"

Akasema, "Ninaamini."

Nikasema, "Kilichotokea, nyuma kule mwanzoni mwa mwezi wa Juni…. Wanajaribu kukushughulikia, na kujaribu kufanya upusuaji kwa ajili ya pingili ya mgongo iliyosogea. Siyo hivyo. Ni neva iliyofinywa. Ulipata hilo kwa kuinua mzigo, ulipokuwa ukifanya kazi kwenye Soko la McSpaddin.

Akasema, "Ninakumbuka wakati ilipofanyika! Ninakumbuka hilo sasa."

Hilo halimponyi. Hilo linaelekeza tu kwenye agizo. Acha kuegemea kwenye bango la ishara; hebu tuendelee mbele kwenye jiji! Hebu tuondoke kwenye huu mlima; hebu tufike kwenye jiji. Hebu tuvuke Yordani!

61 Nimekosea. Nimefanya kosa. Ndiyo sababu nimeweka haya mahubiri kwa jinsi nilivyoyaweka. Kwa sababu, Yeye alisema, "Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe," na wakati huo mkono uliposhuka na kuelekeza kwenye Andiko lile lile…. Kwa muda mrefu nimekuwa nikishangaa, kwa sababu sikujua agizo lilikuwa nini. Nimekuwa nikitafuta kitu fulani cha Kiungu zaidi ya hilo. Mungu hawezi kuondoka kwenye agizo Lake. Mungu hutoa agizo, na hilo ndilo litakalobakia.

Lakini watu wote wa Pentokoste wanapenda ishara. Wanapenda kuiona. Biblia ilisema. "Kizazi kiovu na cha zinaa hutafuta ishara." Lakini agizo lilikuwa "Ombea wagonjwa." Na makumi ya maelefu mara maelfu ambao nimeshindwa kuwaombea ni kwa sababu wote walikuwa na shauku na ishara. Wote waliitamani.

62 Hivi majuzi nilikuwa najaribu kufanyia kazi huduma, nikaingia chumbani. Na mtu Fulani akaja jukwaani, akasema, "Sasa, Ndugu Branhama, subiri kidogo. Suala langu ni tofauti. Ninapaswa tu kujua jambo fulani,"

Nikasema, "Vema, daktari anaweza kukuchunguza."

"Loo, sitaki hilo. Nataka kujua sasa hivi. Suala langu ni tofauti sana."

Nikasema, "Vema, ninachukua kufanya hili, ndugu." Nilienda kwenye hilo, na kitu cha kwanza unajua, Roho Mtakatifu….

Akasema, "Bwana asifiwe! Hilo ni sahihi!"

Nikasema, "Wengine njooni sasa, hebu niombe kwa ajili yenu."

Nilipofanya hivyo, unajua alichokisema yule aliyefuata? "Suala langu ni muhimu tu kama la kwake."

Kisha nikawa nao kama sita au nane, na kufunga mkutano; walitaka kuniua.

Wakati wote nimestaajabu, kwa nini hilo linifanyie hivyo? Ni kwa sababu nilikuwa ninalifanya kwa makosa. Hilo ni bango la ishara tu likielekeza kwenye agizo. Hilo siyo agizo. Hilo bango la ishara limegongolewa chini ulimwenguni. Na lugha—Afrika, India, Asia, Ulaya, ulimwenguni kote—kupitia kwa makumi ya maelfu na mamilioni ya watu, wanajua juu ya bango la ishara. Niko tayari kuondoka kwenye huu mlima. Ninataka kuendelea mbele nivuke Yordani. Ninataka nifikie kitu fulani kule ambapo imani yangu itainuka hadi mahali ambapo nikiombea watu wataponywa.

63 Tazama. Mungu hulirejesha moja kwa moja katika mapaja ya watu: "Ulizaliwa kuombea wagonjwa. Kama unaweza kuwafanya wakuamini…"

Nikasema, "Hawataamini."

Akasema, "Nitakupa ishara mbili, na kwa hizi wataamini." Angalia basi, hizi ishara, wamezikimbiia, bango la ishara, badala ya agizo, wakiamini kuwa "ulitumwa kuomba."

Sasa watu wanapokuja kwenye mstari ili waombewe, mara mmoja anavyolenga shabaha kabisa…. Hakuna chochote ninachoweza kufanya juu ya hilo hadi walenge ile shabaha. Na wanapolenga, ndipo ninasema, "Nakupa…."

64 Hattie Wright, nadhani yuko hapa asubuhi hii. Akiwa ameketi moja kwa moja pale. Alikuwa wa kwanza, tulipowaona wale kindi. Naye alijua agizo kuhusu hilo. Na wakati hizo nyakati saba za mfululizo ambazo Mungu aliumba kitu fulani, nilisema, "Huyo ni Mungu yule yule ambaye aliweza kuumba kondoo dume kwa ajili ya Ibrahimu, ili kumshawishi juu ya agizo lake; ni Mungu yule yule ambaye anaweza kuumba kindi, kwa sababu hilo ndilo lililokuwa hitaji langu."

Na mzee mdogo Hattie Wright pale (akiwa ameketi kule nyuma ya jengo), na moyo ukiwa mbali na vitu vya ulimwengu, alikuwa anaamini. Akasema, "Ndugu Branham, hiyo ni kweli tupu!" Hakulisema tu kutokea *hapa*; Mungu alinena tokea moyoni wake.

Nikasema, "Hattie, omba chochote utakacho. Nitakupa."

Akasema, "Nitapaswa kuomba nini?"

Nikasema, "Unaye baba na mama wazee wakiwa wameketi pale. Unaye dada mlemavu. [Bado yeye ameketi kwenye kile kiti.] Ungeweza kuomba kwa ajili yake. Ungeweza kuomba kwa ajili ya mama yako, baba. Wewe ni masikini, huna fedha zozote. Omba unachotaka."

Akasema, "Vema, sijui cha kuomba." Kasema, "Sijui tu." Kasema, "Shauku yangu kuu ni wokovu wa wavulana wangu wawili."

Nikasema, "Nakupa wavulana wako, katika Jina la Yesu Kristo." Na wote wawili waliongoka, wanampenda Bwana Yesu, wote wawili wakabatizwa katika Jina Lake, na kumtumikia Mungu kila siku kwa mioyo yao yote.

65 Ed Daulton, akiwa ameketi hapa mahali fulani (hapa hapa chini), juu ya watoto wake, jambo lile lile.

Niliona, takriban, katika kampeni, watu mia nane au mia tisa, huenda elfu moja, wakipita jukwaani katika mkutano, mmoja mmoja. Jambo la kwanza unajua, nakwenda na kuwaombea. Hakika wanakuwa wazima. Hapa anakuja msichana mdogo, akiwa anakufa kutokana na saratani ya damu. Hakika nilijua kilichokuwa tatizo la huyo mtoto, kamwe sikusema neno moja kwa yeyote. Lakini yule mtoto alipofika pale, nilisema, "Mpenzi, nakupa shauku ya moyo wako. Una saratani ya damu, na nakupa uponyaji wako katika Jina la Bwana Yesu." Nikageukia mkutano, na nikasema, "Nampa yeyote wenu changamoto hapa, mpeleke huyo msichana kwa daktari, achunguzwe, na mwone kama anayo alama moja ya saratani ya damu." Kwa nini? Yule mtoto alikuwa amesikia. Kama Rahabu yule kahaba, yeye aliliamini hilo kwa moyo wake wote. Ndipo Mungu, kupitia Roho Wake, akarudi nyuma na kusema, "Ndiye huyo." Mamia walikuwa wamepita kwenye jukwaa, kadiri nijuavyo, pasipo kupokea chochote. Niliwaombea tu.

66 Nikarudia watu moja kwa moja, "Kama mtaamini." Agizo lilitolewa. Hilo ni lile la kwanza. Ishara ya

mwelekeo imetolewa. Sasa kama mtaamini hilo, kama mtaamini kwamba Mungu alinituma ulimwenguni kuwaombea wagonjwa, nitaweza kuwaombea maombi ya imani. Hivyo ndivyo tu hilo linaweza kufanyika.

Kamwe Mungu hawezi kutoka kwenye agizo Lake. Nimemkosea. Nimekuwa na kama miaka kumi na nne hapa, pasipo na lolote isipokuwa utambuzi wa moja kwa moja wa siri za mioyo, huko na huko ulimwenguni, hadi maelfu kumi ya nyakati, hali milioni moja, nadhani. Nawauliza jambo moja, je, hilo liliwahi kushindwa? Hapana, bwana. Na kama hiyo ishara ya mwelekeo haiwezi kushindwa, ni kiasi gani zaidi hilo agizo halitaweza kushindwa kamwe! Kama hiyo ishara—hiyo ni sehemu ndogo—kama hiyo ishara inayoelekeza kwenye jiji, kama hiyo haitashindwa kukuambia mji uko kule, ni kiasi gani zaidi hilo jiji litakuwa kule unapokuja! Hilo ndilo agizo.

67 Sasa, huduma yangu I anabadilika. Imekwishabadilika. Bado utambuzi wa siri za mioyo utakuwepo. Itaendelea tu kama tu ninavyojisikia kwamba Mungu anataka niyaseme. Lakini hadi wakati huo, nitawaombea na kuwawekea mikono wagonjwa, kama Yeye alivyoniambia nifanye, na kuchukua agizo langu. Nimesubiri hili kwa muda mrefu, lakini naamini sasa kwamba tuko tayari kuichukua ile nchi ya ahadi. Kwa hakika tu kama kutakavyokuwako, kutakuwako na akina Rahabu fulani wakisubiri, kutakuwako na mtu fulani akingojea ambaye ataliamini hilo kwa mioyo yao yote.

Mnaweza kuelewa? Kila mtu anayelielewa hilo vizuri, inua mkono wako juu. Ni wangapi wanaamini kwamba hilo ni la Kimaandiko kabisa? Hilo ndilo hasa Yeye alilolisema. *Hili* ndilo lile agizo; *haya* yalikuwa ni mabango ya alama za maelekezo zikielekeza kwenye agizo.

68 Sasa, namchagiza mtu yeyote aniambie, kokote ulimwenguni kwenye hizi kanda, anionyeshe wakati mmoja ambapo Yeye aliwahi kushindwa kusema kwenye jukwaa, au nje katika ono lolote au chochote, bali lile lililokuwa jambo sahihi kabisa, likatukia tu kama Yeye alivyosema. Alimwambia kila mtu sawasawa tu yale yaliyokuwa matatizo yao, na yote kuhusu hilo, na walikotoka, na yote ambayo wangepaswa kufanya. Na kila wakati liliposema, 'Hivi Asema Bwana" kwa chochote cha uponyaji, kilitokea namna hiyo. Kama mnajua moja, hebu nijue juu ya hilo. Nitakwenda kwenye hiyo kanda na nione. Halikuwahi kushindwa kamwe, katika hii miaka mirefu kumi na mbili, au miaka kumi na nnea. Halikuwahi kushindwa kamwe, kwa sababu haliwezi kushindwa. Ishara ilitolewa na Mungu. Haiwezi kushindwa.

Na kabla Mungu hajatoa ishara, Yeye hutoa agizo; kabla ishara haijakuwepo ili kuelekeza kwenye agizo. Kabla ya kuwepo na ishara ili kuelekeza kwenye jiji, inapasa jiji liwepo kwanza wa kuelekezea. Kama umeliamini hilo kwa moyo wako wote, utalipokea. "Maombi ya imani yatamwokoa wagonjwa, na Mungu atawainua."

69 Sasa, nimeegemea sana kwenye bango la ishara mwenyewe. Bwana, nionyeshe juu ya hili kabla sijawaombea, kwa sababu sijui ninafanye nini." Hilo lilikuwa la kikatili iliyoje. Naomba kusanyiko linisamehe. Yale makusanyiko ulimwenguni, yanayosikiliza kwenye hii kanda, mnisamehe! Nilikosea. Kamwe sikupaswa kulichukua jambo hilo namna hiyo. Hilo halikuwa agizo Lake kwa kuanzia. Hilo ilikuwa ishara ikielekeza kwenye hilo agizo. Nilipaswa kuwaombea wagonjwa, kila mahali.

Sasa, unaona, hilo limerejea moja kwa moja tena katika mapaja ya hao watu—kama mtaamini kwamba Mungu aliagiza hili litendeke. Hili hapa katika Neno, liko tu kabisa pamoja na Neno, hilo agizo. Na nasema....

70 Nitalichora hilo hapa kwa kidole changu—nusu mviringo , upinde wa mvua. Hilo ni agano Mungu alilolifanya na watu. Yeye alifanya agano na jamii ya mwanadamu asingeangamiza ulimwengu tena kwa maji. Yeye aliweka agano na kila mmoja wa mitume Wake. Yeye aliweka agano na nabii.

Na kule, miaka fulani kumi na tano ... kumi na nne ... kumi na tano iliyopita mnamo 1937, Mei 7, 1937, nafikiri ulikuwa huo, kwamba Mungu aliweka agano na mimi, akisema, "Ulizaliwa katika huu ulimwengu ili kuwaombea watu wagonjwa-kama utawafanya wakuamini." Moyo wangu wakati wote umekuwa kwa ajili ya watu. "Kama utawafanya hao watu wakuamini, na kisha uwe mwaminifu unapoomba, hakuna chochote kitakachosimama mbele ya maombi yako."

Nalisema hilo kwa uaminifu na kwa uso wenye aidu. Kama kuna yeyote anayepaswa kuwa na imani, ingelikuwa mimi—kwa kule kuona kile Yeye amefanya, kule alikonitoa, lile shimo nilikokatwa kutokea humo; kwa kuona kote kwenye maisha kile Yeye alichofanya; kule kuona ninaposimama na kusema jambo fulani, Mungu angekuja moja kwa moja na kuliunga mkono, ukweli.

71 Miaka iliyopita, nilipowaambia kulikuwa na Malaika aliyenijia kichakani nilipokuwa na umri wa miaka mitatu pekee, Nuru, kisulisuli, kikizunguka kichakani, na kuniambia nisivute sigara, nisinywe pombe, au kitu fulani kingine kamwe, kungekuweko na kazi kwa ajili yangu nitakayofanya nitakapokuwa mkubwa zaidi. Mlikuwa na haki ya kulishuku hilo. Hamkuwa na haki, lakini mngeliweza kulishuku hilo.

Chini hapa mtoni, Yeye aliposhuka na kujithibitisha Mwenyewe kuwa hilo, juu kule tulikokuwa tumesimama.... Wengi wenu mlioketi hapa asubuhi hii mlikuwepo mkiwa mmesimama pale. Wengi wenu mnajua hilo ni ukweli.

Wengi wenu mnakumbuka wakati huo wakati lile agizo lilipotolewa, na Yeye akasema, "Nenda, na hii huduma itakwenda ulimwenguni kote, uamsho utaanza." Na kumekuweko na uamsho tokea pale ambao haukuwahi kuwepo. Huo uamsho bado unaendelea, ulimwenguni kote sasa, kampeni kuu za uponyaji ulimwenguni kote.

72 Na mimi, kutokea mtu, asiyefaa kitu. Sisemi hilo kwa kukosa heshima kwa mama yangu akiwa ameketi pale, au baba yangu mpenzi ambaye ameondoka, ambaye maziko yake yalihubiriwa kwenye madhabahu hii. Nililelewa katika familia ya kutisha. Mnajua jambo hilo. Hakuna mmoja wetu Wakristo. Baba yangu alikunywa pombe. Mungu alichukuwa mwana wa mlevi, na angeniosha katika Damu Yake. Nilipokwenda mjini kuongea na mtu fulani, na kuongea na mwanamume fulani, yeye angeliongea na mimi tu kwa sababu hakukuweko na mtu mwingine wa kuongea naye. Mtu fulani angelikuja, tuseme mtu yeyote, haijalishi ilikuwa ni juu ya nini, wangeligeukia mbali na mimi kwa sababu nilikuwa mwana wa mlevi. Na wengi wenu ninyi watu hapa katika kanisa langu mwenyewe mnajua huo ni ukweli. Nilikuwa na jina ambalo kamwe sikuninii ... kama mnyama au kitu fulani. Hata wakati mmoja ilisemekana—wa jijini, kwa mtu aliyekuja nyumbani kwetu—akasema, "Utaambatana na takataka kama hiyo?" Loo, lakini, Mungu, nini ningeendelea nacho isipokuwa Damu ya Yesu Kristo! Sina elimu. Sina hadhi. Sina kitu chochote.

73 Nilimwambia mke wangu siyo muda mrefu uliopita, "Wazia ilikuwaje wakati hakuna mtu angeongea na mimi, nami napenda watu, na wasingenisikiliza."

Ninakumbuka nikiwa ninasoma kitabu fulani, nikienda shuleni…. Niliwapeleka watoto wangu shule hivi majuzi; na niliweza kuwapatia vitabu na vitu, na nilishukuru sana. Mimi ningelienda shuleni bila viatu, nywele zikining'inia shingoni mwangu, hakuna nguo, nimevaa koti dogo la zamani pasipo shati ndani yake, hata sikuwa na kalamu ya risasi au kipande cha karatasi cha kuandika. Ilinipasa kuomba penseli, penseli ya shilingi moja, na kipande cha karatasi ili kuandiki maswali ambayo yalikuwa ubaoni au kitu fulani. Hakukuna chochote. Ilikuwa kosa.

74 Ninakumbuka kusoma katika kitabu siku moja ambapo Abrahamu Lincoln alishuka kwenye mashua kule katika, ninaamini, New Orleans. Akaona kule, wakiwa wamesimama kwenye malisho, watoto fulani wadogo weusi wakiwa na miguu yao midogo mahali ambapo ng'ombe mzee alikuwa amelala usiku kucha, ili kuepuka barafu ardhini. Na alikuwa … walikuwa wamesimama pale wakiimba, "Una viatu, na mimi nina viatu, na watoto wote wa Mungu wana viatu."

Wakati aliposhuka kwenye mashua, alitazama, akiwa amesimama kwenye uzio wa fahalil, hapo alisimama mtu mkubwa mweusi mwenye afya akiwa amesimama pale, mke wake mdogo akiwa na mtoto mchanga mkononi, akilia. Walikuwa wanampiga mnada, kumzalisha na wanawake wakubwa, kutengeneza watumwa wakubwa zaidi.

Lincoln alikunja mikono yake namna *hiyo* na kugonganisha ngumi zake pamoja. Akasema, "Hilo ni kosa!? Kasema, "Siku fulani nitakigonga hicho kitu, kama itachukua maisha yangu!" Kilichukua maisha yake, lakini alikigonga. Naye alikiua hicho kitu.

75 Nikasema, "Huku kunywa, huku kuishi vibaya, ni kosa! Siku fulani nitaligonga hilo!" Nilikuwa niende kuligongaje, nikiwa na jina kama nililokuwa nalo? Hakuna mtu ambaye angelizungumza na mimi. Hiyo ndiyo sababu nilihoji agizo langu. Hakuna mtu aliyenijali. Hakukuwa na yeyote popote, ni miongoni mwa watu wangu hapa tu.

Kwa neema ya Mungu, ilinipasa kuondoka nyumbani kwangu, sitawezi hata kukaa pale, kwa ajili ya kuitwa na watu kote ulimwenguni. Wanaume wa aina zote, watawala, wenye mamlaka, wafalme, watu wakuu, wafanya biashara, wahudumu, kutoka ulimwenguni kote, wakiita. Simu, simu, simu, mchana baada ya mchana, usiku baada ya usiku. Nini kilifanya hivyo? Ni Damu ya Yesu Kristo ambayo inayotakasa nafsi yako. Kama damu ya Abraham Lincoln ilivyovua mkanda wa utumwa wa mtu mweusi, Damu ya Yesu Kristo iliondoa pingu za dhambi kwangu; na kunichukua kutoka kwenye jina la chini kuliko la mnyama, na kuniwekea jina kama mwana wa neema Yake.

76 Na niko tayari kwenda Yordani asubuhi hii. Niko tayari kusimamia agizo langu. Nimewapenda watu. Nimepa watu kilichohitajika. Yeye amekutana na mimi, ono baada ya ono, ambayo sina muda wa kuelezea (na mnajua, yameandikwa moja kwa moja hapa nyuma ya hivi vitabu), yakisema, "Unatoa mno kwa watu. Ili utembee na Mimi, utatembea mwenyewe. Unaweka msisitizo mno juu ya hizi ishara."

Sikujua sehemu iliyobakia ya agizo ilikuwa nini, lakini saa imefika. Saa imekuja wakati ninapoona mkono ukishuka chini kwa Yoshua, kusema, "Nilikuwa pamoja na Musa. Nitakuwa pamoja na wewe." Naliamini hilo asubuhi hii. Kutoka wakati huo, na siku hii na kuendelea, ninamtumikia Mungu katika agizo langu. Kama Yeye anataka kunionyesha ishara au anataka kunionyesha maono, Yeye anaweza kunionyesha hayo. Kama hanionyeshi, kamwe sitasimama mbele ya watu kujaribu kufanya imani yao ivute kitu Fulani kutoka kwangu tena. Nitawaombea wagonjwa na kuwakabidhi kwa Mungu, na kuwaacha waende. Kama wanaamini hilo agizo, Mungu ni mkweli tu. Yeye amenileta umbali huu wote. Kama tu alivyomfanyia Musa, Kama tu alivyomfanyia Yoshua, hilo limefanya vivyo hivyo.

77 Maombi yangu ya unyenyekevu ni, "Mungu, nisamehe. Hebu niinuke na kujaribu tena. Nisaidie, Bwana. Hebu niwaongoze hawa watu, na kuwaweka kwenye Neno, hadi tuweze kwenda hadi Yordani, kwenda katika nchi ya ahadi, pale ambapo kanisa kuu la Mungu lililokombolewa litaokolewa lisitende dhambi tena." Hiyo ndiyo shauku yangu asubuhi hii. Liamini hilo na uishi! Liamini hilo, na uponywe! Nanena nanyi katika Jina la Bwana. Hebu tuombe.

78 Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, mwanzilishi wa Uzima wa Milele, na Mpaji wa kila kipawa chema, hebu rehema na na neema Zako ziwe juu ya mtumishi Wako kwanza, Bwana. Nimefanya makosa mbele Zako kwa kutumia vibaya kitu fulani ambacho kimekuwa cha Kiungu, kwa sababu watu wamekivuta kutokea kwangu, Bwana. Nakuomba Wewe, Ewe Bwana Mungu, kuanzia saa hii na kuendelea, nichochee, Bwana, kwa Roho Wako. Ninaamini kwa moyo wangu wote. Nisaidie wewe kutokuamini kwangu.

Na wakati wanaume na wanawake wanakuja kwa ajili ya kuombewa, kwamba nitalifanya maadam Wewe utanipa pumzi na uzima. Hebu sasa waamini wanapoombewa, Baba. Hebu hili agizo ambalo Wewe umenipa, hebu niweze kulichukua katika ulimwengu wote. Na nitakapofika kwenye sehemu fulani ambapo bango la ishara limegongelewa, hebu wao na wajue kwamba hilo linaelekeza tu kwenye agizo. Hebu na wawe na imani.

79 Bwana, sitasubiri tena kwa ajili ya ishara Fulani au kitu fulani, kiniambie mambo fulani, au ikiwaa *huyu* mtu anakwenda kupona. Nitaenda kukutana na adui kwa imani moyoni mwangu mwenyewe. Nitaenda kumkabili kwa Damu ya Yesu Kristo. Kwa Damu ya Kristo, hawezi kusimama.

Saasa kama mambo haya yote yamekuwa sahihi, ambayo yamethibitishwa kuwa sahihi, hivyo uponye wagonjwa wakati ninapowaombea, Bwana. Ni Neno Lako. Ni ahadi Yako. Ninayo shauku ya kufanya hilo. Nisaidie kutokuamini kwangu.

Nisamehe dhambi zangu, Bwana, za kutokukutii Wewe. Sikujua ni nini tena cha kufanya; kama nilifanya, Bwana, halikuwa limefunuliwa na kuwa wazi kwangu. Sasa limefunuliwa. Ninajua ninakosimamia. Najua agizo langu. Kamwe sitaacha hili Neno liondoke kinywani mwangu, mchana na usiku. Wakati wote nimesimama nalo, Bwana, simama nalo—nikiwaambia watu kwamba kama siyo Neno la Mungu nina mashaka nalo. Lakini nitahubiri au nisifanye chochote isipokuwa iwe ni Neno la Mungu.

80 Lakini, Bwana, ninachoka kutembea huku na huko katika ardhi ile ile. Kama nilivyosema usiku wa jana, miaka arobaini jangwani, kwenda na kurudi, kwenda na kurudi. Mungu akibariki, ndiyo. Kuchunga kondoo na watoto, na chochote zaidi, na makundi na makundi ya mifugo, na zaidi. Mungu, Uliwabariki. Lakini siku moja ulisema, "Mmekuwa kwenye mlima huu muda mrefu vya kutosha. Loo, nendeni kaskazini, kuelekea Yordani."

Mungu, ninaanza hii asubuhi ya leo. Ninaacha haya mabango ya ishara kwa sababu zinaelekeza kuelekea nchi bora. Ninaweza kujikwaa. Ninaweza kupita kwa Waamaleki, naweza kupita kwa Wahiti na Wakanaani, huenda nikawapitia wanaonikosoa mimi binafsi. Bwana, nitaendelea tu kusonga mbele kwani najua kuna nchi kule mahali fulani. Kuna mahali fulani, hali fulani, mahali fulani ambapo tunaweza kwenda tufike pale ambapo utajibu maombi, kwamba chochote tutakachoomba tutapewa, siyo hata saratani itakayosimama mbele ya hayo maombi. Najua hilo kuwa ni kweli. Kwamba ninaamini na kulisubiria, Bwana. Na najisalimisha mwenyewe Kwako asubuhi hii kwa ajli ya huduma Yako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

81 Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu.

Sasa kanda ilizimwa, kwa sababu hili litaenda ulimwenguni kote. Hilo ni kutoka moyoni mwangu. Mnaweza kuelewa, kanisa?

Mungu kamwe hawezi kusema kitu chochote na akikatae. Maneno Yake hayashindwi. Ahadi Zake ni za kweli. Wakati huu wote amekuwa akisubiria hii saa. Ona, ni maombi ya imani yanayomwokoa mgonjwa, siyo ishara. Maombi ya imani! "Kama utaamini," Yesu alisema, "Ninaweza. Ninaweza, kama ukiamini." Sasa kama Mungu amenipa nguvu za kuomba maombi ya imani juu yako, na ameliahidi hilo na kuthibitisha kuwa ni kweli, sasa unaamini? Kile ninachoomba, ninapokea, kama ukiamini hilo. "Kama unaweza kuwafanya watu waamini, na kuwa mwaminifu unapoomba, hakuna chochote kitakachosimama mbele ya maombi yako."

82 Ndugu, dada, kama niliwahi kutataka kuwa mwaminifu, ni sasa. Baada ya makosa yangu yote, katika kuonyesha, ninachotaka … sababu ya kuleta hizi jumbe huko nyuma, kwamba Mungu anaonyesha hapo kwamba Yeye ni mwingi wa rehema. Musa alifanya makosa yake, mtu mkuu kama yeye. Kisha Yoshua alipokuja, alikuwa afanye yak wake pia. Lakini Mungu akasema, "Kama nilivyokuwa na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe."

Sasa mtazame Mungu, miaka miwili iliyopita, akielekeza hilo Andiko moja kwa moja kwangu. "Kama

nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe. Sitaangalia makosa yako." Yeye alijua kwamba hii saa ilikuwa inakuja. Sasa iko hapa. Ona, imerudi moja kwa moja tena, kwa sababu Mungu kamwe hawezi kuondoka kwenye hilo.

"Mmeokolewa kwa imani." Wangapi wanajua hilo? Haijalishi ni watu wangapi wazuri wanakuombea, ni wahubiri wangapi wazuri wanaokuhubiria, unapaswa uwe na imani yako kibinafsi kwa ajili ya wokovu. Je, hilo ni sahihi? Ni nini yako mwenyewe…. Sijali ni mahubiri mangapi mazuri unayoyasikia, wewe ni wa makanisa mangapi mazuri, ni imani yako kibinafsi inayokuokoa. Unalia kwa sauti kiasi gani, unaomba kiasi gani, unapiga kelele kiasi gani, unacheza katika Roho kiasi gani, unaokolewa tu na imani yako. Je, hilo ni sahihi? Hiyo ndiyo njia pekee unaponywa kwayo.

83 Kama Mungu akimpa mtu ujumbe, mhubiri, mhubiri anahubiri wokovu na hutoa ujumbe, unaona huo ujumbe kuwa ni kweli, Mungu huuthibitisha kwa Neno Lake, kwamba hiyo ni kweli; basi ni kiasi gani unapaswa kuamini zaidi hiyo karama ya uponyaji, inapokuwa imekwishathibitishwa kwa Neno na kwa malaika, kwa ishara mbili ambazo zilizoelekeza kwenye kutokushindwa kwa zote mbili? Ni kiasi gani unapaswa kuamini! Ona, na maadam….

Ili kuonyesha kwamba haikuwa mapenzi makamilifu ya Mungu kabisa kufanya hivyo, hiyo ishara wakati wote ilinidhoofisha. Wangapi wanajua hilo? Mwuulizeni mke wangu nyuma kule. Anaweza kuwaambia. Ndiye—hugongana na hilo vibaya sana kuliko wengine—inampasa kuchukuliana na mimi. Bila kujua hasa pale ulipo, na unakotembea, na *hili, lile*, na una [maneno yasiyosikika vizuri]. Unakwenda barabarani kipande kidogo, na kusimama.

84 Sasa, nikija kutoka kwenye hii mikutano iliyopita, niliwachukua hao watu kwenye mstari. Kwanza: tungekuwa na jioni mbili huru, pasipo kutoa kadi za maombi. Kisha inakuwa ni msururu ikatupasa kutoa kadi za maombi. Ningesimama wakati fulani na kufanya hamsini au sabini na tano, labda arobaini au hamsini, utambuzi, kwa wakati mmoja; na kila usiku. Je, hilo ni sahihi, Gene, Leo, na ninyi mlioko hapa, mlioko kwenye mkutano? Hakika, ilikuwa kweli. Na hilo lilifanya nini? Liliponiacha, na nikaanza kwenda nyumbani, ningelisahau mahali nilipokuwa, nikitaka kujua mahali nilikotokea kwenye njia kuu.

Sasa unamaanisha kuniambia Mungu humfanyia mtu hivyo? Hapana, bwana. Ilikuwa ni mtu akijifanyia hilo mwenyewe, kwa kuchukua bango la ishara badala ya agizo. Nilisimama chini ya mti mdogo wa zamani kule, pembezoni mwa barabara, mahali fulani huko Washington, au mahali fulani kule. Nikasema, "Bwana, kama tu utaniruhusu nijirudie mwenyewe, vyema tena, nisaidie kujua kweli ni ipi, ili niweze kuwa sawasaw na watu tena, na kupata agizo sawasawa."

85 Ninalo sasa. Nikiwa nimeketi chini hapa kwenye mteremko wa mlima wa Kentucky hivi majuzi, kukiwa kumekucha asubuhi moja, Yeye alinifunulia hilo. Na ndilo hili. Ndilo hili. Sasa ninaenda katika Jina la Bwana Yesu. Ndilo hilo.

Liaminini hilo, na muishi! Liaminini hilo, na mpone! Siwezi kumfanya yeyote aamini hilo. Unapaswa uliamini hilo mwenyewe. Lakini nimewaambia ukweli. Mungu amelishuhudia hilo kwamba ulikuwa ukweli kwa njia ya Neno Lake, kwa njia ya malaika Wake, kwa njia ya ishara na maajabu, kwa miaka mirefu kumi na mbili. Kama hawataliamini hilo sasa, kamwe hawataliamini. Je, hilo ni sahihi? Lakini saa imekuja wakati ambapo nimechoka kukaa kwenye huu mlima. Ninataka kwenda hadi Yordani. Nataka kuingia kwenye ahadi kamilifu. Nataka kupata imani ndani yangu mwenyewe, siyo kuangalia kwenye ishara, siyo kuangalia kitu fulani ambacho Mungu amekifunua, au aina fulani ya bango la ishara. Nataka kutazama kuelekea Kalvari na niseme, "Nakuja, kwa iman, Bwana Mungu. Ninakuja katika Jina la Bwana Yesu.

86 Sasa kuna baadhi ndani hapa wa kuombea asubuhi hii, Nakuja kukabiliana na ugonjwa na mateso ya mwili wako katika Jina la Yesu Kristo. Nitafanya hilo mpaka Mungu atakapochukua uzima kutoka kwangu. Maadam ananipa hisia na ufahamau nitakuja kuomba. Usishindwa kwa kile unachokiamini—kwamba ninapokuombea, unakwenda kupona. Hakikisha hilo. Kama huamini hilo, basi usije kabisa, kwa sababu utajiumiza tu mwenyewe.

Sasa liko kwenye kanda, na liko hapa. Kutoka hapa na kuendelea, hakuna utambuzi tena hadi Mungu amenipa ninii … aniambie nifanye kitu fulani; niende kumwambia *huyu* mtu jambo fulani, ndipo nitaenda kuwaambia. Yeye aseme fanya jambo *fulani*, nitakwenda nilifanye.

Lakini maadam nimesimama pale, "Sasa nitazame. Unaamini kwa moyo wako wote. Ndiyo, hili ni *Fulani*. Wewe ni *John Doe*, umetokea sehemu *fulani*. Ulikuwa na saratani kwa muda *fulani*. Daktari *Fulani* alikwambia hutapona. Ulikwenda na kufanya jambo *fulani*. Sasa unapaswa kukichukua na kukirudisha *hicho* na kulitengeneza *hil*i, na ulipate *hili* kabla ya kupona. Vema, Ndugu *Doe*, endelea sasa, liamini hilo." "sasa, wewe ni dada *Fulani*, umetokea sehemu *Fulani*." "Umetokea sehemu *Fulani*." Na kisha ninaingia kwenye kisulisuli, nikiwa sijui la kufanya, hasa. Na jambo la kwanza unajua, ndani hapa kuna mwingine, ninatazama nione ni nani ninamtazama. Na natoka nje ya mkutano, na "Mimi niko wapi?" Hukuna zaidi ya hilo.

87 Nakuja katika Jina la Bwana Yesu, kama mtumishi Wake. Kama Mungu hajawathibitishia hilo hadi wakati huu, kwamba nimewaambia ukweli, basi kamwe hamtaamini kwamba nimewaambia ukweli. Amina. Hilo ni sahihi. Ni kweli. Wangapi wanataka kuombewa, inueni mikoni yenu juu. Vema.

Sasa ninamhitaji Teddy. Teddy bado yupo ndani ya jengo? [Mtu fulani anasema, "Hapana, alilazimika kuondoka."] Alilazimika kuondoka. Ni nani ambaye ni mpiga kinanda hapa ambaye angeweza kunipigia wimbo *"Amini tu"*? Kama utaweza, kama kuna mtu fulani hapa ambaye anaweza kupiga? Umeupata huo … au, unao ukiwa umerekodiwa, unao, mahali fulani? Kama kuna mtu yeyote hapa ambaye anataka kutupigia, *"Amini tu,"* mpiga kinanda fulani, njoo moja kwa moja mbele. Mwanamume au mwanamke, haijalishi, tutafurahi kukupata. Sawa kabisa, sasa wakati unapiga taratibu, kama utapiga, dada mpenzi.

88 Sasa hatutatoa kadi za maombi. Tunapokuwa kwenye mkutano mdogo kama huu, hatuitaji. Tunapokuwa kwenye mikutano mikubwa, bado tutapaswa kutoa kadi za maombi, kama nikiombea mia tano. Bado utapaswa kutoa, kwa sababu unakuwa na wengi sana katika … kutembea huku na huko katika msongomano, unaona.

Wangapi wanaamini kwamba haya ni mapenzi ya Mungu? Loo, kitu fulani kinanifanya nijisikie nimefanya kwa usahihi, kitu fulani kinafanya…. Kimeondoka kwenye kifua changu. Kimekuwa pale kwa miaka kumi na mbili, nikijua kumekuwa na kitu fulani cha makosa, Ndugu Lee. Sasa najua kimeondoka pale. Nimesema hilo, limerekodiwa, na kimeondoka kwenye kifua changu sasa.

89 Kumbuka, unaweza tu kuokolewa kwa imani yako binafsi. Unaweza tu kuponywa kwa imani yako binafsi. Je, mnaamini hii kuwa ni Biblia? Neno la Mungu! Je, mnaamini mchungaji wenu kwamba ni mtu wa Mungu, kanisa lolote unaloenda? Kama huamini, unapaswa kuliacha. Nenda kwa mtu ambaye ni mtu wa Mungu. Kisha kama unamwamini, amini kuwa anakuambia ukweli, kisha uikubali. Imani yako binafsi katika Kristo inakuokoa. Haijalishi mchungaji wako ni mzuri kiasi gani, mama yako, alivyo wa mtauwa, mtakatifu, jinsi Neno la Mungu lilivyo halisi, unalia kiasi gani, unaomba kiasi gani, ni imani yako ndiyo inayokuokoa! Umeokolewa kwa imani.

Sasa kitu kile kile kinatumika. Haijalishi namna…. Neno la Mungu linasema kwamba Yeye angetuma hili katika siku za mwisho. Mahubiri mawili ya kufuatana sasa, nimewaleta Israeli wa kimwili na Israeli wa kiroho pamoja. Tunamtafuta Yoshua wa siku hii, ambaye ni Roho Mtakatifu, atuongoze kwenye ile nchi. Inampasa Yeye anene kupitia mtu fulani, kwa sbabu Yeye ni Roho. Nimewaambia kile Yeye alichoniambia. Sasa aminini, na mponywe.

90 Sasa hebu hawa, upande *huu* wa mstari, Doc, nenda chini kule. Billy Paul, Billy yuko wapi? Njoo hapa umsaidie Doc, kama utaweza.

Na sasa kila mmoja wenu anayekuja kupitia huu msitari wa maombi, kumbuka, litakurudia moja kwa moja kama hutaamini kwa moyo wako wote. Ni kweli. Lazima uliamini hilo. Sasa kumbuka, ni wewe ambaye ni mgonjwa. Mungu amelisema hilo katika Biblia Yake, Mungu alilituma kupitia kwa mjumbe Wake, Mungu alilithibitisha kupitia kwa malaika Wake, sasa ni lazima uliamini.

Sasa ninyi mnaotaka kuombewa, Biblia ilisema hili hapa, "Kama wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Na hilo ni kweli. Na tunataka kuamini hilo, kwa mioyo yetu sasa, na Mungu atajalia uponyaji wako.

91 Sasa njooni kwenye njia *hii*, moja kwa moja hapa, na mrudi moja kwa moja nyuma; hebu upande *huu*, kisha upande *huu* mwingine mrudi kwa njia ile ile. Hebu upande ule wasimame upande wa mkono wa kuume, hapa. Vema. Unasema nini? [Mtu fulani ananena na Ndugu Branham.] Ninaenda kushuka moja kwa moja chini hapa. Ndiyo, bwana, moja kwa moja chini hapa kuwaombea.

Sasa hizi barua na leso, nimeviombea. Wengine wenu, baadhi yenu, labda mnaweza kuondoka. Msisahau usiku wa leo, sasa, ibada itakuwa juu ya uthibitisho, *Uthibitisho Wa Kiungu Kwa Kanisa La Kweli*, mnaona?

92 Sasa kwenu ninyi mnaokwenda kuombewa, je, mnaamini kwa hakika kwamba mtapona? Kama huamini, usije. Kama unaamini, ni wajibu wako kuja.

Sasa, mimi siyo mponyaji, lakini nina karama ya uponyaji. Hilo lilishuhudiwa. Limethibitishwa kwamba hilo ni kweli. Ona, nyuma huko, muda mrefu uliopita, nakumbuka nilizoea kwenda hospitalini hapa. Na nilikuwa tu mhubiri wa Kibaptisti, hapa eneo husika. Ningelienda hospitalini. Palikuwa na nesi mzee pale, aliishi katika Howard Park. Sijui kama bado yuko pale au la, pale hospitalini. Alizoea kumwambia mgonjwa, "Sasa unaenda kupona. Sasa naenda kupona." Kasema, "Yule mhubiri mdogo wa Kibaptisti anakuja kukuombea." Ona, ilikuwa ninii tu … ilikuwa mwanzo. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Na sasa ilikuwa inaenda kutawanyika, kutokea mahali hapa, kote ulimwenguni.

93 Na sasa Yeye amenipa hizi ishara kuzifanya elimu yangu, sasa, kama nilikuwa na elimu ya baadhi ya hawa wahubiri wengine (kwa mfano, mmoja ninayemjua, labda kama Ndugu Neville, au Dr, Vayle, baadhi

ya hao), nisingepaswa kuwa na hii. Lakini nilipaswa kuwa nayo, ili kufanya hili, ili nishughulike nalo mahali pa kile ambacho sikuwa nacho katika upande wa elimu. Ilinipasa niwe na ishara. Na ninii tu…. Hizo ishara zimethibitika tu kuwa na mafanikio kama ambavyo elimu ingefanya. Lakini, mnaona, kama huna sifa, Mungu anaweza kukupa sifa kwa njia nyingine.

Sasa, mmwe na Imani na muamini. Sasa, nataka kila mmoja wenu amwahidi Mungu, pale uliposimama. Kwa sababu, kama hutamwahidi, halitakusaidia. Nataka kila mmoja wenu aweke pembeni kila kivuli cha mashaka. Na unapokuja mstarini, ninapokuombea, ninawataka mtoke hapa…. Huenda usione nukta moja ya matokeo. Lakini Yesu kamwe hakusema, "Je, umeliona? Je, ulilihisi?" Yeye alisema, "Je, uliliamini? Je, uliliamini? Kama mkiamini…."

94 Sasa nimeona hili njiani. Nawaombea watu, baadhi yao Yeye asingefanya huo utambuzi, wangelienda zao wakisema, "Loo! Sikupata kitu chochote. Yeye hakuniambia kitu chochote." Huyo mtu kwa kawaida wala hakupata kitu chochote.

Lakini baadhi yao wanakuja mstarini wakisema, "Asante, Bwana. Ninaliamini hilo." Hao ndio walioniambia: "Unajua, Ndugu Branham, kamwe sikusikia tofauti yoyote kwa siku kadha [labda wiki mbili au tatu au zaidi], lakini mara nilianza kuhisi kile kitu kikiniacha." Na hicho kikaondoka, unaona.

Unaweza kusema unaamini. Kuna madaraja matatu ya watu wanaohudhuria mikutano—hao ni wasioamini, waamini wa kujifanya, na waamini. Baadhi yao hujifanya kama wanaamini: "Loo, ndiyo, ninaamini," Lakini hawaamini. Kama unaliamini hilo…. Nataka kukuuliza hili swali sasa. Kama unaliamini, hakuna uwezakano wewe kutokupona. Sikiliza. Hebu nirudie hilo. Kwa ujumla haiwezekani usipone, kama unaliamini hilo.

95 Kwanza, Neno la Mungu hutoa agizo. Mnaamini hilo? Neno la Mungu husema hivyo kwanza. Hilo ni juu ya kila kitu. Jambo la pili, malaika wa Bwana amelithibitisha hilo, ishara zimelithibitisha hilo. Je, hilo ni sahihi? Sasa, hakuna kushindwa hata mara moja kokote.

Hakuna kushindwa hata mara moja katika Neno la Mungu, lililosema, "Niliwahi kuwapa uponyaji wakati mmoja, lakini sasa ninawaondole." Nataka mtu fulani anionyeshe hilo. Nitawaonyesha pale ambapo Yesu aliagiza kanisa Lake kuombea wagonjwa, na maombi ya imani yatamwokoa huyo mgonjwa. Sasa mniambie pale lilikosema lisingeweza kutokea tena. Nionyesheni katika Biblia, unaona.

Yeye alisema katika siku za mwisho Yeye angefanya haya mambo fulani, kuinua haya mambo. Tazama kile kilichokuja kutimia. Yeye ametimiza Neno Lake. Sasa, nimewaambia kwamba aliniagiza. Sasa, ulimwengu unalijua hilo, sayansi inalijua hilo, yule Malaika wa Bwana analithibitisha hilo, na matokeo yamethibitisha kwamba hilo ni ukweli.

96 Tunaishi kwenye ulimwengu mgonjwa. Wapo wengi wa kuombewa. Nilifikiri kwa hakika kuna njia fulani nyingine mbali na….

Ndugu Moore aliniambia wakati mmoja…. Kulikuwa na masikini msichana mdogo akitambaa kwenye jengo, mlemavu. Jamaa mdogo masikini, akijaribu kufika nilikokuwa. Nikatazama chini. Yule mtoto mtoto akaanza kulia. Vema, hawakuweza kumleta kwenye mstari, hakuwa na kadi ya maombi. Bila kujua huo ulikuwa ndio usiku wa mwisho wa huyo mtoto, na Ndugu Moore na wengine wakamsaidia kutoka kwenye mstari.

Siku iliyofuata tuliketi na kulizungumza. Yeye akasema, "Ndugu Branham, hilo linaniumiza."

Nikasema, "Linakuumiza? Unafikiri lilifanya nini kwangu?"

Ona, msichana mdogo mlemavu. Hilo lilining'ang'ania. Na hilo lilikuwa kiasi cha miaka kumi iliyopita, msichana mdogo mlemavu kule Illinois, kichwa kidogo cheusi, macho ya kahawia, akitambaa, ugonjwa mdogo wa polio akijaribu kufika mahali nilikokuwa. Na mabawabu chini pale walilazimika kumsaidia na kumrudisha aketi kwenye kiti chake. Akatambaa kutoka kwenye kiti chake ili afike pale. Kwa nini? Unaweza tu kuchukua kiasi fulani. Na nilikuwa nimepunguza baadhi yao, kumweka ndani pale bila kadi ya maombi, wengine wangekuwa wameumia hisia zao, ona. Hilo ni sahihi, singeweza kufanya hilo. Nikasema, "Hakika kuna njia fulani nyingine." Natamani ningekuwa nimejua wakati huo kile ninachokijua sasa. Mambo yangelikuwa tofauti. Hakika yangekuwa tofauti.

97 Sasa, kila mmoja wenu, kitu pekee ambacho kitakuzuia usiponywe ni wewe kutokuamini hilo.

Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu.

Baba yetu wa mbinguni, hapa wamesimama vipofu, walemavu, wanaoteseka, wagonjwa, wanaokufa kwa saratani, vidonda vya tumbo, uvimbe. Wote wamesimama hapa kwenye mstari, Bwana. Nimehubiri Neno. Na kwa miaka kumi na mbili umelithibitisha kote ulimwenguni. Nimeomba msamaha. Na ninajua sikulifanya hilo kwa kudhamiria; nilifanya kwa sababu nilifikiri ninafanya sahihi. Sasa nakuja, Bwana, naja kwako kwa unyenyekevu, nikikuomba ubariki maombi yangu, kwamba nitakapoomba kwa ajili ya hawa

watu, kila mmoja wao atapona. Bariki imani yao. Saidia kutokuamini kwetu, Bwana.

Na hebu kila mmoja asubuhi hii akamate hilo ono hasa. Hebu wasipoteze chochote katika hilo, lakini wapate kuliona Kimaandiko. Na kumwazia yule Malaika wa Bwana nyuma kule mwanzoni, alisema, "Kama Musa alivyopewa karama mbili…." Na kisha miaka miwili iliyopita, ukileta Biblia; kwa mkono unaoshuka kwenye… kama lililoandikwa kwenye ukuta kule Babeli. Mkono wa mwanadamu, ulionekana kama, ambao ulielekeza kwenye Biblia hadi kwenye mlango huu huu, "Kama nilivyokuwa na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe." Na, Baba, hili hapa asubuhi hii, limeletwa kwenye nuru. Tunakushukuru kwa ajili ya hili, Bwana. Unisemehe makosa yangu.

Na sasa tunapokwenda kwenye huu mkutano wa maombi, hebu nguvu za Mungu ziponye kila mtu mgonjwa atakayekuja kwenye mstari. Naenda tu kama mtumishi Wako, siombi upako wowote maalum, kitu chochote maalum, lakini nikijua hili, kwamba katika maisha yangu ni hilo agizo. Naenda kulichukua, katika Jina la Yesu Kristo.

98 Sasa, Ndugu Neville, kama utasimama hapa. Sasa, kwa hii karama, siendi kupaka mafuta, ona. Naenda tu kufanya kile Yeye alichoniambia nifanye. Kama agizo lilivyosema, "Wafanye watu wakuamini, na uwe mwaminifu." Mnaamini? Basi mimi ni mwaminifu. Inapasa kitu fulani kitukie!

Ndugu Neville anaenda kuongoza katika nyimbo. Wote mwombe kimya kimya ninappombea wagonjwa. [Ndugu Neville anaanza kuimba "Amini tu."]

99 Bwana Yesu, ninaweka mikono juu ya mwanamke mwenye haya mawe ya kwenye figo, na ninayakemea katika Jina la Yesu Kristo. Hebu aenda na akaponywe. Amina. Kitu fulani kilitokea.

Shida yako ni nini?

Bwana, ninaweka mikono yangu juu ya ndugu, shida hii ya tezi dume, na nakemea hii nguvu ya pepo katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Lazima upokee. Amini.

Bwana, pamoja na shida ya moyo na magonjwa mengine, ninaweka mikono yangu juu dada yangu, na kukemea hili katika jina la Yesu, kwa agizo langu.

Bwana, naweka mikono yangu juu ya dada yangu akiwa nah ii miguu mibaya iliyovimba. Nakemea huko kuvimba katika Jina la Yesu Kristo. Nenda, amini hilo, dada, nawe utaliona.

Bwana, akiwa na shida ya moyo na magonjwa mengine, naweka mikono yangu juu ya dada yangu, na kukemea hili katika Jina la Yesu, kwa njia ya agizo langu.

Bwana, akiwa na kuona kunakoshindwa na shida ya moyo, nalikemea hilo katika huyu mwanamke, kwa agizo langu kutoka kwa Mungu, katika Jina la Yesu. Amina. Inapasa iwe hivyo! Itaenda kuwa sawa. Ni sawa kabisa. Amina. Naliamini kwa moyo wangu wote.

100 [Nafasi katika kanda] Hilo ni kweli, kama ni wakati wako kuondoka, unapaswa kwenda njia fulani. Hilo ni sawa. Lakini, kwanza, kabla Yeye hajakwambia, kama utakuwa mwaminifu na usitilie shaka hilo, utapona. Hilo ni sahihi kabisa.

Lazaro alifufuliwa kutoka kwa wafu. Alikufa tena, lakini alifufuliwa kutoka kwa wafu, ili kuonyesha kwamba Mungu hutimiza ahadi Yake kwa watu. Yeye alisema, "Mariamu, unaamini hili? Mimi ndiye huo ufufuo na uzima. Nimeagizwa na Mungu kufufua wafu. Unaamini hili?"

Mariamu akasema, "Naam, Bwana. Naamini kwamba wewe ni Mwana wa Mungu ajaye ulimwenguni."

Kasema, "Mmemzika wapi?" Ona?

Ilimpasa kufa tena. Lakini Yeye alimfufua kuonyesha kwamba Yeye alikuwa ufufuo na Uzima.

Ona, Mungu hufanya hayo mambo, na kila kitu kiko katika utaratibu wa Kiungu. Loo, ninafuraha sana kusema hilo! Kila kitu kiko katika utaratibu mkamilifu. Kama mtaamini, kila kitu mtakachoomba mmepewa. Inapaswa iwe hivyo.

101 Vema, endeleeni tu kuomba sasa wakati tunapowaleta. Mungu akubariki…?...

Bwana Yesu, dada yetu ni mgonjwa sana, akiwa ananisikia nikisimama hapa na kuhubiri haya maneno. Hebu huku kusuasua kidogo kwa mashaka kuondoke tu mbali nao wote, Bwana. Hebu wainuke, waache huu mlima wa kale wa kwenda nyuma na mbele, waendelee kwenda Yordani, Bwana.Tujalie hilo, Bwana. Hebu dada yetu asafiri njia hii sasa, kutokea saa hii na kuendelea, akiamini kwamba Mungu anaponya mwili wake. Katika Jina la Yesu. Endelea njiani ukiamini.

Mungu akubariki. Bwana Yesu, mpe shauku ya moyo wake kwa ajili ya binti yake na familia yake. Naomba hilo katika Jina la Yesu atapokea hili, ninapotoa maombi yangu na imani yangu kwa kuweka

mikono juu yake. Kama sikukuamini Wewe, singeweka mikono yangu juu yake. Kama nilijua hutalitenda, nisingemwombea. Lakini naamini, Bwana, na yeye anaamini, pia, na tunaweka imani yetu pamoja, tukiamini katika Yesu. Amina.

102 Mungu akubariki, Pat. Bwana, kwa ajili ya watoto wake wa thamani anataka waokoke. Anapata ugumu katika kusikia. Daktari anasema kuna mtoto wa jicho akitokea kwenye jicho lake. Yeye anahitaji kuishi kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Mjalie hilo, Bwana, ninapoomba kwa ajili ya hii rufaa kwa ajili ya ndugu yangu. Amina.

Mungu akubariki, ndugu. Usitilie shaka. Amini hicho ambacho umeomba.

Bwana, huyu mwanamke mdogo masikini akiwa asimama hapa kwa ajili ya mwanawe. Ningetaka … kwamba uta [maneno yasiyosikika vizuri] kitu fulani, Bwana, kinachomuumiza. Anaendea kupandikiziwa ngozi. Na anaomba kwa ajili ya mwili wake na wokovu wake. Anaombea wapenzi wake. Ameomba kwa ajili ya hali yake mwenyewe ya wasiwasi, Bwana. Amekaribia tu kuvunjika. Mungu, ninaomba kwamba utampa shauku ya moyo wake. Mponye na mateso yake, na kumfanya kuwa mzima. Katika Jina la Yesu ninaomba maombi haya ya imani juu yake. Amina. Mungu akubariki, dada. Nenda ukiliamini hilo. Mungu akubariki.

103 Bwana, kwa ajili ya wokovu wa wapenzi wake. Naomba kwamba utamjalia ombi lake. Katika Jina la Yesu. Amina.

Amina sasa, dada, kwamba umelipokea hilo, na ni lako. Kama unaamini hilo, linapaswa litimie.

Kwa ajili ya ndugu yetu Edgar Tyler. Barikiwa moyo wako! Vema, na njia yote tokea Phoenix, Arizona. Ni joto kule?

Yule bibiye hapa aliponywa kwenye mkutano wangu. Alitokea wapi? Unatoka Phoenix, bibiye? Wewe hutokei…. Ulikuwa kule Phoenix, mkutanoni.

Unataka Yeye akufanyie nini, bwana? Akuondolee pumu. Mungu akubariki, ndugu.

Mungu mpenzi, kama ambavyo huyu ndugu wa thamani [maneno hayasikiki vizuri] piga kelele [maneno hayasiyikiki vizuri] na kwa ajili ya mizigo ya watu. Ninaomba kwamba utamjalia ukombozi; akija kote kutokea Phoenix, Arizona, kuombewa, kusimama katika huu mstari, kusikia Ujumbe, kumtia moyo. Bwana, inaonekana kama kujitolea kukubwa. Ni hivyo.

Lakini yule Malkia wa kusini alikuja kwa miezi mitatu mgongoni mwa ngamia kupitia jangwa la Sahara ili kusikia hekima ya Solomoni; na tazama aliye mkuu zaidi kuliko Solomoni yupo hapa. Roho Mtakatifu yupo hapa, aliye mkuu kuliko Solomoni.

Bwana, naomba kwamba utamponya haya mateso ya mwili wake. Mpe shauku ya moyo wake. Hebu atembee katika njia aliyowekewa. Hebu wema wa Mungu ukae juu yake. Naomba baraka hizi kwa ajili ya ndugu yangu katika Jina la Yesu Kristo, Mwana Wako. Amina.

Ed, unaporudi nenda na hilo. Ni la kwako. Nakupa hilo. Nenda na ulipokee.

104 Ndugu George. Karibu kila mmoja anamfahama George Wright. Ni wangapi wanaikumbuka ile habari, alipokuwa anakufa hivi karibuni? Madaktari wote walimpita. Mwili wake ulikuwa umevimba namna hiyo, kuganda kwa damu moyoni mwake. Madaktari kadha walikuwa wamemkatia tamaa. Nilienda kumwombea. Ndugu Funk (alikuwepo hapa kitambo kidogo kilichopita, ninaamini) alikuwa pamoja nami kule usiku huo. Tuliketi juu ya kilima kule, niliigiza kama nilikuwa nakwenda kuwinda.

Nataka kuliambia hili kanisa sasa, inanipasa kusema mambo fulani ambayo yamekuwa yakiendelea. Mara nyingi mnafikiri ninawinda, mimi siwindi. Hilo ni udhuru ili kuzuia watu wasiwe wananifuata. Inanilazimu kwenda kule kuwa mwenyewe na Mungu. Siko tu huko nikiwinda, marafiki. Ndiyo, mimi nawinda, lakini siyo hiyo aina ya uwindaji.

Niliketi juu ya kilima. Sasa, kwake yeye nilikuwa nakwenda kuwinda sungura. Tulienda moja kwa moja kuzunguka nyuma ya nyumba, na nilitoa mikono yangu na kuishika kuelekea kwenye nyumba na kuomba na kuomba. Nikiwa nakufa! Roho Mtakatifu alinena nami usiku mmoja, "Mmoja wa hawa wanaume anatoka kwenye kanisa ambalo haliamini kuwa uponyaji ni sahihi."

Mhudumu fulani alikuja yumbani kwake siyo mrefu uliopita na kujaribu kunipinga pale kwa majadiliano. Wengi wenu ninyi watu hapa mlikuwepo usiku ule. Mliona pale yule mtu karibu arukwe na akili zake? Na sasa anajaribu hatimaye kumpata Roho Mtakatifu. [Ndugu Wright anasema, "Ambapo anasema mimi ni rafiki bora aliyenaye, hata hivyo,"] Wazia hilo.

105 Mtu ambaye alisimama pale kubishana, na kusema, "Kwanza nataka kukuambia, wewe ni wa Ibilisi."

Nikasema, "Nakusamehe kwa sababu hujui unachokizungumzia."

Kisha wakati huo akageuka na kusema, “Ninajua unaye Roho wa Kristo.”

Nikasema, “Nilikuwa Ibilisi dakika chache zilizopita, na ni Kristo sasa. Ni kipi? Hivyo sasa … mambo ya kutisha yametokea.

*Huyu* mtu akiwa amelala pale akifa, na huyu mtu akamcheka, kasema, “Sasa mwendee mponyaji wako wa Kiungu.”

Na nilikuwa kule Lexington, Kentucky, ambapo mwanamke aliponywa saratani. Na Bwana akanionyesha kwenye ono, nikiwa ninarudi asubuhi ile kwenye saa kumi na moja, Yeye alinionyesha kwamba … kasema, “Utapeana mkono na Ndugu George Wright, akiwa anakuja Hekaluni, na kutembea hadi juu hapa na kumpa mkono wako. Na yule mtu aliyemdhiaki, atachimba kaburi lake.” Sikulijua hilo, sikujua yeye alichimba makaburi.

106 Nikampigia simu Dada Wright. Anapaswa kuwa hapa mahali fulani. Naam. Nilimpigia simu Dada Wright, nikasema, “Nina 'Hivi asema Bwana.'” Vema. Hayo ndiyo aina ya maono ninayotaka kuyaona kuanzia sasa na kuendelea; [maneno yasiyosikika vizuri] Nimwambie mtu jambo Fulani, lirudi. Nikasema, “Ndugu George atachimba kaburi la huyo mtu, au atakuwa kwenye kaburi la huyo mtu, ambaye alikuwa anamdhihaki. Na yeye atakuja Hekaluni, na nitapeana naye mkono.” Kuganda kwa damu kukamwacha Ndugu George.

Na takriban mwezi mmoja au miwili baada ya hilo nilirudi. Na yeye wakati wote, karibu kila wakati, huja kupitia njia *hii*. Lakini asubuhi ile alikuja kupitia mjia *hii*. Kusanyilo likasema, “Tazama, tazama, tazama, huyu hapa anakuja moja kwa moja kuushika mkono, kabisa tu kama ilivyokuwa.

Na yupo hapa leo. Hilo limekuwa [Ndugu Wright anasema, “miaka tisa”] miaka tisa iliyopita. [“Nilikuwa vibonge tisa vya damu iliyoganda vilivyobaki.”] Vibonge tisa vya damu iliyoganda, miaka tisa iliyopita!

107 Hata hivyo, nasikia kwamba Dada Hickerson…. Je, Ndugu Heckerson yupa hapa leo? Dada Hickerson ana hali nzuri zaidi, hilo ni jema. Alikuwa na kuganda kwa damu, pia, lundo la hivyo kwenye mguu wake.

Sasa Ndugu Hickerson ana baridi yabisi katika mkono wake.

Huyo alikuwa binti yake, Dada Hattie aliyeketi pale, ambaye nilitoa ushuhuda wake, sasa, kwamba ile huduma mpya ilifanya kazi kwa mara ya kwanza. Hilo ni sahihi, Dada Hattie. Sijui kama wavuna wako ndani hapa asubuhi hii, wako pamoja na wewe? [Dada Hattie anasema, “Kule nyuma.”]

Hao wavulana wako wapi? Hao hapo wote wawili wakiwa wamesimama pale pale nyuma kule nyuma. Hao hapo wavulana wawili. Huyo ni mama, binti wa ndugu yetu. Inueni mikopo yenu juu, wavulana, ili waone ninyi ni akina nani. Sawa, wamesimama nyuma kule. Ni zuri sana, sivyo, Orville? Hakika ni zuri.

108 Vema.

Ndugu George. [Ndugu Wright anasema, “Unajua, Ndugu Bill, naamini.”] Najua unaamini. Na najua, mara nyingi nimelala pale chumbani mwako, wakati wa usiku, nikitazama nje dirishani, nikisikiliza ndege mwimbaji wa kale. Siku fulani tunapaswa kwenda kule, Ndugu George. Hadi wakati huo, Mungu awe pamoja nasi. Ninajua Yeye atakuwa pamoj nasi. “Naam, nijapopita katika bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya, Wewe uko pamoja nami.” Katika lile ono hapa siyo muda mrefu uliopita, nilipowaona hao watu wazee wamegeuzwa kuwa vijana tena, hivyo ndivyo nitakavyowaona ninyi siku fulani, kamilifu.

Baba yetu wa mbinguni, mpe ndugu yetu shauku ya moyo wake. Mponye na hii baridi yabisi. Yeye nazeeka, Baba, na ninaomba kwamba utamsaidia. Msaidie Dada Wright na Edith mdogo, na familia yote kule. Dada Hattie na watoto wake, wapenzi wao wote. Uwe pamoja nao, Baba. Jalia hili ombi, ninapoomba katika Jina Yesu. Amina.

[Ndugu George Wright anasema, “Nitakuwa na miaka sabini na tisa.] Sabini na tisa. Mungu akubariki, ndugu Wright, na akupe siku nyingi zaidi. Bwana asifiwe.

109 Ndugu Daulton. Jamani, jamani! Hapa kuna ndugu ambaye amekuwa wa thamani kwangu. Nitawaambia ni nini kilichotokea. Sijapata muda wa kulipitia hilo. Mke wake anajua. Alisema alikuwa anakufa. Shambulio la moyo, ilikuwa hilo, dada? Na kabla, Bwana alimpata mke ndoto, na fasiri ikaja. Na shambuo la moyo lilipompiga mume, dada alisimama moja kwa mbele yake na kusema, “Ninapinga hili!” Mungu alikuwa amempata ndoto kwamba itakuwa hivyo, na fasiri ikaja. Na daktari alifikiri yule mwanaume alikuwa anakufa wakati huo, na yeye yupo hai hapa leo.

Bwana Yesu, kwa ajili ndugu yetu wa thamani, aliyeendesha gari umbali mrefu kuja kwenye huu mkutano asubuhi hii. Nyonga yake ni mbaya. Kama tu gari, Bwana, viungo vinaanza kuchakaa, vikishuka, lakini, Ewe Bwana, uwe nguvu zake. Wewe ndiyo nguvu zetu. Funga hii sehemu iliyolemaa kwenye nyonga yake. Funga kila sehemu dhaifu, Bwana. Na mpe ndugu yetu wa thamani uponyaji wake, ninapombariki katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao. Amina.

Mungu akubariki, Ndugu Daulton. Na iwe hivyo.

110 Vema, dada, Mungu anaweza kukufanyia nini? [Dada ananena na Ndugu Branham.] Mbona, Dada Daughterty! Je, huyu ni Betty? ["Huyo ni mimi."] Mbona, Betty, barikiwa moyo wako! Ni nani katika hili Hakalu asiyemjua Betty Daugherty! Mara ya kwanza huduma yangu ya zamani kufanya kazi ilikuwa kwa huyu mtoto. Wangapi wanakumbuka kuhusu nguo?

Betty alikuwa na dansi ya St. Vitus. Na alikuwa katika hali ambayo hakuenenda kama mwanadamu. Hakuna daktari ambaye angeweza kufanya chochote kwa ajili yake.

Na nilienda St. Louis. Hili kanisa liliandaa fedha, na niliazima koti la mtu fulani, na walitafutia dola kumi na moja kwa ajili yangu, ili niende kule kumwombea huyu msichana mdogo. Alikuwa tu msichana mdogo, kama huyu msichana mdogo aliyeketi hapa, msichana mdogo. Na nilikaa (Ndugu Daugherty yuko hapa? Hayupo.) na niliomba na kuomba na kuomba. Nisikuweza kwenda popote. Na hatimaye, nikiwa nimeketi huko nje ndani ya gari la Ndugu Daugherty, niliona ono kuhusu ni nini wao wafanye.

Na alifuata hilo ono kabisa tu jinsi Bwana alivyosema afanye. Naamini ilikuwa kidogo kinyume na mawazo yao kwa wakati huo. Lakini alilifanya tu sawasawa jinsi Bwana alivyosema alifanye, na Betty aliponywa. Mara ya kwanza kumwona, jinsi…. Kasema, "Akavuta …Daugherty mmoja upande mmoja wa mwisho wa kitanda na Ndugu Daugherty ule mwingine, na Dada Daugherty akachukua tambara na kumnawisha mtoto uso na mikono, na kadhalika." nilipoinama chini kenye maombi, "Baba yetu uliye mbinguni, Jina Lako litukuzwe."

111 Na Betty sasa amepigwa na mtoto wa jicho. Ilinipasa kumwombea muda mfupi tu uliopita, nyuma ya jengo kule Chatauqua

Betty, mpenzi, hebu twende kwenye hili kwa karibu hasa sasa. Nataka kushika mkono wako. Je, huoni kabisa, Betty? ["Hapana."] Unaweza tu kuona mwanga wa mchana na giza likiingia. ["Hilo ni sahihi."] Una umri gani, Betty? ["Ishirini na mbili."] Ishirini na mbili. Alikuwa na umri wa kama miaka saba au nane wakati huo. Dada Daugherty, umekuwa na kuvuta kugumu, sivyo? Unajua, Betty, wakati wote nimeamini kwamba Mungu alikuwa na kitu fulani kwa ajili yako kufanya. Na naamini ndiyo sababu imekuwa namna hii kwako. Na sasa naamini kwamba adui amefanya hili jambo ovu.

Sasa, unajua, Betty, hii. Kama ningelikuwa na uwezo wa kufika ndani pale na kushika huyo mtoto wa jicho na kuvuta nje, ningefanya hivyo. ["Ndiyo."] sina huo uwezo.

Lakini, Betty, kile nilichokuambia mara ya kwanza, huo ndiyo ukweli, kama ninavyoketi hapa, na wewe na mimi, kama ndugu na dada katika Kristo. Ndugu Daugherty, baba yako wa thamani, akiwa ndugu mtamu tu niliyewahi kuwa naye. Mama yako mpenzi hapa. Nimeishi kwenye nyumba yenu, na tumeshirikiana chakula chenu, na kila kitu. Umekuwa namna hiyo kama vile ulikuwa dada yangu kabisa, na nisingeweza kuwa mwaminifu zaidi kuliko ambavyo ningekuwa pamoja na Dolores aliyeketi nyuma pale.

112 Sasa, Mungu aliahidi hili, Betty. Nataka kutoa yote…. Baba yako, akiwa mhudumu, umelelewa katika familia ambayo huombea wagonjwa. [Maneno yasiyosikika vizuri.] Umeombewa mara nyingi. Imefikia mahali mbapo wakati mwingine unapita tu juu yake, kwenda nyuma na mbele, na ni kama tunapoteza thamani ya hilo. Unaona kile ninachomaanisha?

Jamani, umekuwa msichana mzuri, mrembo, Betty. Ni aibu kuona macho yako yamekuwa namna hiyo. Je, Meda bado yuko ndani ya jengo? Mke wangu alitaka kukuona. Ninataka akuone, Betty, amekuwa mtoto mrembo iliyoje. Betty, ulikuwa msichana mdogo mrembo. Wakati wote umekuwa msichana mwema.

Sasa, kuna mambo machache katika maisha ambayo ulikosea, Betty? Sasa, ni kama tu vile daktarin angeutazama mwili wako wa asili, ninataka kuangalia nafsi. Umemkosea Mungu popote, Betty? Kama uliwahi, kiri tu hilo Kwake: "Bwana, kama utaniruhusu kulipitia hilo tena, nitafanya tofauti."

113 [Betty Daugherty ananena na Ndugu Branham.]

Jamani, hili ni jambo la ajabu. Hebu tulifikirie na-namna hii. Sasa, sikujua kwamba Betty Daugherty angekuwepo kwenye huu mkutano. Lakini wa kwanza katika utambuzi wangu mwingine alikuwa ni Betty Daugherty. Huu hapa umerudia tena, kwenye mkutano wa kwanza juu ya jambo hili.

Alijua wakati huo huo kile nilichoongelea. Sitaki kuanza utambuzi huo tena, kwa sababu katika mstari…. Lakini alisema kile alichopaswa kusema sasa hivi tu. Alijazwa kwa Roho Mtakatifu nje kule St. Louis. Akiwa msichana tineja, watoto, huenda amefanya mambo ambayo hakupaswa kuyafanya. Lakini ni hajafanya? Ni nani hajafanya? Kama siyo neema, wote tumepotea. Na kama uko tayari kukiri makosa yako, Mungu ni wa haki kukusamehe makosa yako.

114 Ninainua imani yangu sasa. Bwana, ninamlete huyu msichana Kwako. Na ninaweka mikono yangu juu ya macho ayke. Ninakemea huyo mtoto wa jicho, na kuamini kuwa yataona tena. Hebu nguvu za Mungu aliye hai, aliye wa Kiungu, mpe Betty kuona kwake tena, ninapotoa haya maombi wakati imani ikiwa juu

yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Hebu nipeane mkono na dada yangu tena mahali fulani, leo, kesho, au popote itakapotokea tena, na hayo macho maangavu yaniangalie na kusema, "Ndugu Branham, naweza [Maneno yasiyosikika vizuri] kuona vizuri tu kama nilivyowahi kuona…."

[Maneno yasiyosikika vizuri.] Je, unaamini hilo, Dada Daugherty? Basi litakuwa hivyo!

Bwana, katika jina la Yesu, Mwana wa Mungu, mpe dada yetu shauku ya moyo wake, anapokuwa amesimama tayari kusikia kutoka Kwako. Hebu ile nguvu iliyomponya Betty Daugherty mara ya kwanza, na mara hii pili pia, hebu imponye dada yetu, katika Jina la Yesu. Amina.

115 Ndugu… [Ndugu anazungumza na Ndugu Branham] Ndugu yetu anataka kuokolewa. Je, unamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wako binafsi? Je, unaamini kwamba alikufa kwa ajili yako, na kufufuka tena? Je, sasa unamchukulia Yeye kama Mwokozi wako binafsi?

Katika Jina la Yesu Kristo, hebu kila suala la dhambi liondoke katika dhamiri ya huyu mtu. Hebu ndugu yetu [maneo yasiyosikika vizuri], tutoeka sasa na kuendelea, maisha yake sasa ni ya Kikristo, katika Jina la Yesu Kristo.

Geukia hili kusanyiko na useme, "Ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu." Sasa kwamba yeye anafurahi sana dhambi zake zimesamehewa kwa Damu ya Yesu Kristo! Hilo ndilo tunalopenda, amina, uponyaji maradufu, kwa kupigwa Kwake. [Nafasi tupu kwenye kanda.] Bwana, mpe huyu mwanamke uhakika wa wokovu wake. [maneno yasiyosikika vizuri]' katika Jina la Yesu Kristo unapaswa kuliamini hilo. Enenda ukiamini sasa. Usitilie shaka.

116 Na kwamba nimefanya mengi asubuhi ya leo—kwa ujumbe niliokuwa nao na mambo kama nilivyokuwa najua, nimefuata hilo agizo-zaidi ya nilivyofanikiwa katika miaka mitano iliyopita, kwa sababu nimepata kiini cha mapenzi ya Mungu.

Sasa, inaweza kuwa kitu kigumu kwangu kubadilika kutoka huduma moja hadi nyingine. Lakini, siyo kubadilisha huduma, ni kuchukua huduma ile ile katika kiwango cha juu zaidi. Ni agizo la awali. Haya mambo mengine yote yamekuwa yakijengwa juu ya hilo. Sasa ni wakati.

Kwa moyo wangu wote, ninaamini kwa ajili ya kila mtu ambaye nimemwombea. Ninaamini wanakwenda kupona. Na kwa ushahidi wote ambao tunao, kila kitu ambacho Mungu ameonyesha, mwaka baada ya mwaka, kwa udhibitisho usioshindwa, wa Biblia ikiwa hai tena, basi ni vipi litashindwa? Haliwezi tu kushindwa.

117 Sasa, kuna namna moja tu ya kufanya lishindwe, hiyo ni kwa wewe kutokuamini. Kama Yesu alisimama hapa Mwenyewe, na akuombee, na apitie matendo yale yale ambayo tumeyapitia asubuhi hii, hakuna ambacho kingetokea zaidi kama ungeliamini kwa kipimo sawa cha imani. Hakuna ambacho kingetokea zaidi kuliko ambacho kingetokea kama unaamini kwa kipimo kile kile cha Imani. Kwa sababu, mimi ninamwakilisha tu Yeye. Mimi ni mwenye dhambi niliyeokolewa kwa neema, mwanadamu tu kama wewe, mwanadamu tu. Lakini inampasa Mungu awe na pitio mahali fulani. Na Yeye amethibitisha hilo kwa njia ya Neno Lake. Yeye amethibitisha hilo kwa njia ya hiyo huduma. Yeye amethibitisha hilo kwa njia ya Malaika wa Bwana, na ndilo hili hapa. Sasa ni juu yetu kuliamini hilo.

Sasa kumbuka, kama tu mtoto. Kama kumekuweko na mateso, usiyaone tena. Kama umekuweko na ugonjwa, haupo hapoe tena. Puuza tu dalili yoyote, kitu chochote ambacho ni kinyume kwa kile ambacho kimeombwa. Mara nyingi…. Kila mtoto ajaye kwa Mungu, lazima ajaribiwe. Tunajaribiwa, kuona kama tunaliamini hilo au la. Na utakuwa na vita na shida, lakini kumbuka tupo safarini.

118 Mungu akubariki. Ninawapenda. Na kwa msaada wa Mungu, ninatumaini ataniruhusu niwahudumie kama mtumishi Wake kwa mngi, miaka mingi ijayo, ni maombi yangu. Niombeeni.

Na sasa kumbukeni usiku wa leo: *"Vithibitisho Vitano Visivyoshindwa Vya Kanisa La Mungu Aliye Hai."* Hadi wakati huo, hebu na tusimame kwa miguu yetu, kitambo kidogo tu.

Loo, je, kuna ibada ya ubatizo? [Ndugu Neville anasema, "Ninaamini upo."] Loo, ibada ya ubatizo—watu kwa ajili ya ubatizo, mko hapa? Inua juu mkono wako, mtu yeyote kwa ajili ya ubatizo. Moja, mbili, Tatu…. Ndiyo. Ninasikitika sana, sana, marafiki.

Sasa kwa wale ambao watapaswa kwenda, nitawaruhusu. Hao wengine mkae kwa ajili ya ubatizo, ambao wananataka. Tutakuwa na ibada ya ubatizo, kitambo kidogo tu.

119 Baba Mungu, waruhusu hao wanaolazimika kwenda, wakiwa na baraka Zako, Baraka Zako, neema Yako ikae juu yao, wakikushukuru kwa yote yaliyofanyika asubuhi hii, tunapojivuta mbali na mlima, tukianza kupanda. Bwana, hebu tutembee kupitia kila kiwango cha ngazi, hadi tufike kwenye Ufalme wa Mungu. Tujalie hilo, Bwana. Uwe pamoja nasi sasa. Tusamehe dhambi zetu, hao wanaobaki sasa ili kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao, katika Jina la Yesu Kristo. Na hebu tujaliwe mambo haya.

Tukusanye pamoja tena usiku wa leo. Hebu nguvu Zako na Baraka Zako ziwe juu yetu usiku wa leo. Hebu pawepo na usiku mkuu leo. Hebu wengi waliochanganyikiwe wakanyooshwe usiku wa leo. Tujalia hilo, Baba, kwani tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Vema, mnaweza kuketi sasa kama mnapenda, wakati tunajiandaa kwa ajili ya ubatizo.

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7